# UWEKEZAJI

Asanteni, sana. Kwa hakika ninaihesabu hii kuwa moja ya sehemu muhimu za maisha yangu, kuwa hapa katika jiji hili kuu la New York, kuzungumzia tawi hili, au matawi haya, hasa, nikiwa na wakati huu kuketi jukwaani pamoja na ndugu zangu wahudumu, na kuwazungumzia wanaume na wanawake wafanyabiashara wa jiji hili, kuhusu Bwana wetu Yesu Kristo. Hapana shaka ila wengi wenu mnamjua Yeye, kutokana na tendo lenu asubuhi ya leo, na kushangilia na kumsifu Yeye kwa ajili ya wema Wake na rehema.

2 Ninajisikia mdogo sana hapa, kusimama hapa pamoja na hawa wazungumzaji mashuhuri na inanibidi kusimama hapa na kuzungumzia kusanyiko hili, kwa sababu mimi si mnenaji mzuri, daima nimesema kwamba mimi ni tairi la akiba. Unajua, unatumia tairi la akiba wakati una moja ambalo halina pumzi; bali hatuna lolote lisilo na pumzi, ila wameacha tu tairi la akiba likimbie kwa dakika chache, nadhani.

3 Nilikuwa nikizungumza kuhusu, ndani ya nafsi yangu, dakika chache zilizopita, na nia, kuhusu . . . kuhusu kuzaa tunda la Roho, kama ndugu mmoja alivyotoa nukuu hiyo, "kuzaa tunda." Mnajua, hatuwezi kutengeneza tunda. Inatubidi kuzaa tunda. Unaona, kondoo hatengenezi sufu; lakini kwa sababu ana sufu, na hutoa sufu, yeye ni kondoo. Hiyo ndiyo sababu yeye hutoa sufu. Hiyo ndiyo njia pekee tuwezayo kuwa Wakristo, si kwa sababu kwamba tuna jina, ama kujaribu kufanyiza kitu fulani, kukitengeneza. Kwa kuwa kondoo, unatoa tu sufu. Kwa kuwa Mkristo, unazaa tu matunda yake. Naam.

4 Na tukiketi asubuhi ya leo, ninajua muda wetu ni mfupi katika mikutano hii.

5 Sababu nyingine ya sisi kuwa New York kwenye wakati huu, nilisikitika kwamba sikuweza kuhudhuria mkutano huo. Rafiki yangu mpendwa sana alinielewa vibaya, wakati aliposema, "Je! utazungumza kwenye mkutano huko New York?" Bw. Williams. Ninaishi Tucson, Arizona; yeye anaishi Phoenix, Arizona, imeachana kwa yapata maili mia moja na ishirini tu. Ndipo nikasema, "Naam, nita—nitakuwa huko Novemba, nitafurahia kufanya hivyo," kukutana na Ndugu Nelson, Ndugu Sweet, na rafiki zangu hapa. Na nikaja kugundua, ilikuwa Oktoba. Na Oktoba nilikuwa niwe Alaska, kwa hiyo nilikuwa mbali sana na New York wakati huo.

6 Lakini kupata majaliwa haya ya kuja hapa pamoja na Ndugu Vick wa Kanisa la Mwamba, na wahudumu, na sisi tuko hapa chini katika Ukumbi wa Marc, ambapo tumekuwa na wakati mzuri juma hili, tukiona Ufalme wa Mungu miongoni mwetu.

Tuna furaha sana kwa hilo. Ndipo basi kuja kwenye wakati huu asubuhi hii, ambapo labda wanaume, wafanyabiashara wanaume na wanawake kutoka kwa matabaka mbalimbali maishani, wameketi hapa; Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Katoliki, na chochote kingine.

7 Inanikumbusha miaka iliyopita, wakati nilipokuwa nikifanya kazi kwenye ranchi ya ng'ombe huko juu Colorado. Nilikuwa. . . tungewaondoa ng'ombe. Shirika la Herefodi hulisha kwenye bo—bonde, nalo huitwa Shirika la Herefodi la Mto Msumbufu. Ranchi yetu ndogo ilikuwa juu upande wa juu wa mto. Na tulikuwa na East na West Fork, na sisi tulilishia East Fork. Ndipo basi majira ya kuchipua ya mwaka, tukiondoa ng'ombe kwenye malisho basi, na kuwaweka juu kwenye Msitu wa Arapaho, ambapo Shirika hulishia.

8 Sasa, ni Shirika la Herefodi. Kuna watu wengi, katika Shirika pale, ambao hufuga ng'ombe wa Herefodi. Na kama ranchi yako inaweza kutoa tani mbili za nyasi kavu, unaruhusiwa, kwa chapa, kuweka ng'ombe kwenye malisho kwa ajili ya majira ya kiangazi, ili kwamba nyasi zako ziweze kukua mahali wanamwagilia maji, na kuwalisha kote katika majira ya baridi.

9 Sasa wakati tukiwa na ukusanyaji wa majira ya kuchipua, na kuwapeleka ng'ombe mbio kwenye malisho, kuna uzio wa kutangatanga. Uzio wa kutangatanga ni ambapo ng'ombe hawatangatangi na kuingia kwenye—kwenye shamba la kibinafsi, yuko kwenye shamba la serikali. Naye mhifadhi daima anasimama kwenye uzio huu wa kutangatanga, naye huwaangalia ng'ombe wanapopita. Vema, zipo chapa nyingi ambazo hupitia kwenye mwa—mwanya huo, au uzio mdogo.

10 Na kuna, vema, Bw. Grimes ni mmoja wa wahifadhi wakubwa, alikuwa na kile wanachokiita Mkuo wa Almasi. Alikuwa na maelfu kadhaa ya ng'ombe. Na Turkey Track, na Lazy K, na wengi juu chini huko. Walipitia.

11 Nilisimama mara nyingi, ama kuketi, hasa, kwenye tandiko, huku mguu wangu ukiwa juu ya pembe ya tandiko, na kumwangalia huyo mhifadhi akitazama ng'ombe hao wakipita. Na jambo la kushangaza, yeye kamwe hakuangalia chapa kwenye ng'ombe. Hakuangalia. Wote inabidi wawe ni Herefodi la sivyo hawawezi kuingia mle. Na kitu cha pekee alichoshughulikia, kama ilikuwa ni Herefodi au sivyo; si aina ya chapa waliyokuwa wamevaa. Kuna kitambulisho cha damu kwenye sikio, ambacho kilionyesha kwamba walikuwa ni Herefodi.

12 Nami nikawaza tu, kwamba ndivyo itakavyokuwa kwenye—kwenye mkusanyiko mkubwa wa kuingia katika Ufalme wa Mungu. Yeye hataangalia chapa, kama sisi ni Methodisti, Baptisti, Presbiteri. Bali Yeye ataangalia kitambulisho cha

Damu. Hiyo ni kusema, sisi sote lazima tuwe na kitambulisho cha Damu, "Kwa kuwa nionapo Damu, nitapita juu yako." Mwanadamu amejaribu kuelimisha watu ili kuingia ndani ya Yesu Kristo; tumejaribu kuwaingiza kwa hotuba. Bali Mungu anayo njia moja, hiyo ni chini ya Damu, tuna mambo shirika.

13 Wakati fulani uliopita, familia fulani ilikuwa inatengana. Ndipo wakili akawaambia ni afadhali waende chini wagawane mali yao kabla ya talaka kuruhusiwa, kwa sababu kusingekuwa na chochote kingebakia kama mawakili wakiishika. Kwa hiyo ilitokea kwamba alikuwa rafiki yao binafsi. Basi wakaingia kwenye chumba kimoja, sebuleni, mume na mke, na wakagawana, na kuzozana juu ya kile kilichokuwa humo ndani. Na chumba kilichofuata, wakazozana tena. Hatimaye wakapanda juu kwenye dari, upenu wa kale, wakapata kasha huko juu, na walikuwa wanagawana mali iliyokuwa humo ndani; mmoja akinyosha mkono na kunyakua, "Na *hicho* ni changu! Na *hiki* ni changu!"

14 Ndipo hatimaye waliinua kijitambaa fulani, na wote wakashika kitu fulani. Basi waliposhika, walishikana mikono. Na chini ya mikono hii kulikuwa na jozi ya viatu vya mtoto, ambaye alikuwa ni matunda ya ndoa yao, ambaye Mungu alikuwa amekiita maskini kitoto hicho Nyumbani. Hakuna mmoja angeweza kudai hiyo, maana ilikuwa ni mali yao wote wawili. Walikuwa wamepata kitu walichokuwa nacho shirika. Basi hapo, wakitazamana usoni, haikuchukua muda mrefu mpaka walikuwa wamekumbatiana. Na talaka haikutolewa, wangeweza kuifutilia mbali, kwa sababu walipata kitu walichokuwa nacho shirika.

15 Nafikiri hicho ndicho tunachopaswa kupata. Kuna kitu kimoja. Huenda sote tusikubaliane kuwa Methodisti, au Baptisti, au Pentekoste, au hivyo, bali kuna kitu kimoja tulicho nacho shirika; Yesu Kristo, tuna Yeye shirika.

16 Mtu fulani aliniuliza, wakati fulani uliopita, kasema, "Kwa nini unaambatana na hawa Wafanyabiashara wa Full Gospel? Unadhaniwa kuwa mhubiri."

Nikasema, "Vema, mimi ni mfanyabiashara."

Kasema, "Ati mfanyabiashara?"

Nikasema, "Naam, bwana, mimi—mimi ni mfanyabiashara."

Kasema, "Uko katika biashara gani?"

Nikasema, "Hakikisho la Uzima wa Milele."

17 Kamwe sikusema *bima*. Nilisema "hakikisho." Kama yeyote wenu anataka hiyo hati ya mkataba, hakika ningependa kuzungumzia hiyo na wewe, punde tu baada ya mkutano.

18 Inanikumbusha wakati nilipokuwa shuleni, kama mvulana, tulikuwa na rafiki huko, alikuwa ni rafiki mwema sana, alikuwa ni mwuza bima. Na kwa namna fulani, sina chochote dhidi ya

bima, sasa, bali sina tu yoyote ya bima hii ya duniani. Kwa hiyo wakati fulani uliopita, jamaa huyu kijana . . . Ndugu yake ni mhudumu wa Kibaptisti, pia, na yeye huandika makala katika ninii cha *Juu* . . . kwa ajili ya *Chumba Cha Juu*. Na yeye akaja katika nyumba yangu, na akasema, "Vema, Billy, kwa hakika nina furaha kupata kukuona tena."

Nikasema, "Kaa chini, Wilmer."

19 Tukaanza kuzungumza. Na mimi nilijua alichokuwa anakujia. Nina kaka yangu ambaye huuza bima, lakini kamwe sikuchukua yoyote, hata hivyo. Kwa hiyo akasema, baada ya sisi kuzungumza kidogo, akasema, "Nasikia, Billy, kwamba huna bima yoyote," akasema, "na nilifikiria labda ningezungumza na wewe kuhusu hati ya mkataba. Na . . . "

20 "Loo," nikasema, "asante, Wilmer, lakini nina ha—hati ya mkataba iliyolipiwa."

21 Ndipo akasema, "Loo, samahani," akasema, "ni hati ya aina gani uliyo nayo, Billy?"

Nami nikasema, "Uzima wa Milele."

22 Basi amini usiamini, mvulana huyo akasema, "Sidhani kama ninaifahamu Kampuni hiyo." Anasema, "Makao yake makuu yako wapi?"

Nikasema, "Utukufuni."

"Loo," akasema.

Nikasema:

> Ni hakikisho lililobarikiwa, Yesu ni wangu!
> Loo, ni kionjo jinsi gani cha utukufu wa Kiungu!
> Mimi ni mrithi wa wokovu, nimenunuliwa na Mungu,
> Nimezawa kwa Roho Wake, na kuoshwa katika Damu Yake.

23 "Loo," akasema, "hiyo ni nzuri sana, Billy, ila hiyo haitakuweka hapa juu makaburini."

24 "Lakini," nikasema, "itanitoa." Sina wasiwasi kuhusu kuingia ndani. Naam. Amina. Sina wasiwasi kuhusu kuingia ndani. Ni, kutoka.

25 Kwa hiyo ni—nina furaha sana kuwa na hakikisho hili kwamba nitatoka huko. Kwa sababu, Yeye ambaye aliandaa hati ya mkataba, kwamba sote tuweze kutoka huko, nimepokea hakikisho hilo moyoni mwangu, kwamba nimepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Nami ninajua, siku moja, kwamba Yeye atanitoa huko.

26 Sasa kabla tu hatujalikaribia Neno, ningependa tuinamishe vichwa vyetu na kuzungumza na Mwandishi, kwa muda mfupi tu, kama mnaweza.

27 Na huku tumeinamisha vichwa vyetu na macho yenu yamefumbwa, na ninatumaini mioyo yetu imeinamishwa, pia, katika Uwepo Wake. Sijui, sasa hivi, kama kuna yeyote hapa ndani ambaye kwa kweli hana hakikisho kama hilo la ufufuo, limefichwa katika kasha la usalama la moyo wako, asubuhi ya leo, na ungetaka kukumbukwa katika maombi? Hivi utaninii tu, pasipo mtu yeyote kuangalia, inueni tu mikono yenu, na kusema, "Nijumuishe na mimi, ndugu." Asanteni, asanteni. Bwana awabariki. Madazani ya mikono wakati tukiomba.

28 Mungu wa Neema nyingi, Baba wa Milele wa Bwana wetu Yesu Kristo, Yule ambaye alimfufua Yeye katika siku ya tatu baada ya kusulubiwa Kwake, kwa kutuhesabia haki, amemwasilisha Yeye kwetu katika umbo la Roho Mtakatifu ambaye sasa anakuja akibariki mioyo yetu na kutuhudumia sisi mambo ambayo tunahitaji katika safari ya maisha haya.

29 Tukitambua na kuona mikono hii ikiinuliwa, Bwana, kuna haja kubwa miongoni mwetu, asubuhi ya leo. Pia ninaomba, Mungu, kwamba Wewe hutamwacha hata mmoja wa watu hao atoke hapa bila ya kuwa na hakikisho hili, kwamba dhambi zao ziko chini ya Damu, nao wamezaliwa tena, na kutiwa muhuri katika Ufalme wa Mungu, kwa Roho Mtakatifu. Tujalie, Baba.

30 Tubariki basi tunaposikiliza Neno Lako. Tunajua Neno Lako ni Kweli, na hakuna Kweli nyingine nje ya Hilo. Pia tunaomba, Baba, kwamba Neno Lako litakuwa halisi kwetu, leo hii. Kwa kuwa imeandikwa, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, nalo Neno lilikuwa pamoja na Mungu, nalo Neno lilikuwa Mungu. Na Neno likafanyika mwili likakaa miongoni mwetu. Yeye yule jana, leo, na hata milele!"

31 Na Yeye ametuambia kwamba "kazi" ambazo Yeye alifanya, sisi tutazifanya pia, kwa sababu Uhai Wake uko ndani yetu. Tena tunaomba, Baba, kwamba huu utakuwa ni ufahamu mzuri kwa kila mmoja wetu, asubuhi ya leo. Na kama tunaweza kukiri asubuhi ya leo kwamba Shakespeare aliishi ndani yetu, tunajua tungeweza kufanya kazi zake, kutunga mashairi. Kama kazi, au uhai, hasa, wa Beethoven uliishi ndani yetu, tungekuwa Beethoven, tungetunga nyimbo. Lakini tunapokiri kwamba Uhai wa Yesu Kristo uko ndani yetu, Uzima wa Milele, basi Uhai wenyewe utashuhudia kile tulicho. Na kama vile ndugu amenena kuhusu—kuhusu kule "kuzaa tunda," tunajua Uhai wa Kristo ndani yetu utazaa ushahidi kwamba Yeye yupo hapa. Kwa hiyo tunaomba kwamba Wewe utajalia tukio hilo kwa kila mmoja wetu, asubuhi ya leo, tunapongojea.

32 Kufungua Neno Lako, hatuwezi kulifungua Hilo. Tunaweza kugeuza ukurasa na kusoma, bali ni Roho Mtakatifu pekee anayeweza kuchukua Neno na kuligawanya Hilo mioyoni mwetu kama tulivyo na haja. Na kwa unyenyekevu tutakusifu Wewe,

kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu, Mwana Wako mpendwa. Amina.

33 Ningewatakeni nyinyi, ikiwa mnazo Biblia zenu; na mara nyingi, watu wanapenda kuhudhuria ibada, na halafu wanasikiliza kile mhudumu anachosoma. Kwa sababu, hata hivyo, Neno la Mungu ni Kweli. Hakuna kweli yoyote nyingine inayoweza kuchukua mahali Pake. Lote ni Kweli. Neno ni Mungu, Hilo ni Mungu katika umbo la maandishi.

34 Mungu anaenda kuuhukumu ulimwengu siku moja kwa Yesu Kristo. Tunajua hilo.

35 Hawezi kuuhukumu kwa kanisa. Kama ingekuwa hivyo, Katoliki ya Rumi ilisema, "Yeye atauhukumu kwa kanisa letu," basi vipi kuhusu Katoliki ya Kiyunani? Methodisti inasema, "kuuhukumu kwa kanisa letu," basi vipi kuhusu Baptisti? Kwa hiyo unaona kuna tofauti kubwa sana.

36 Hapana budi kuwe na kigezo fulani. Na ikiwa Yesu Kristo ni Neno, basi Yeye atauhukumu kwa Neno. Kwa hiyo chochote Mungu alichosema katika Neno Lake, hicho ndicho tunaishi kwacho. "Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

37 Hebu tugeukie Marko Mtakatifu, mlango wa 10, tusome tu sehemu ya Maandiko.

38 Na wakati mnapofungua, ningependa kuwaalika kwenye ukumbi. Lakini niliona tamasha la kuhuzunisha jana jioni, hata nilipoondoka kwenye teksi, ama kutoka kwenye teksi, hasa, kwenda mimbarani. Kulikuwa hasa na maelfu wakitembea chini mtaani, wengi wao wakilia, kwa sababu walikatazwa kuingia kwenye ukumbi. Hakukuwa na nafasi. Tunasikitika tusingeweza kupata mahali popote pakubwa zaidi. Lakini tunatumaini, siku moja, ikiwa sote tunaweza kuja kuona . . . tusipofanya hivyo, tutawaoneni tu ng'ambo ya mpaka, upande ule mwingine.

39 Sasa cha 17 cha mlango wa 10, kuanzia na cha 17, kwa ajili tu ya fungu dogo, kufanya . . . kutoa kutoka kwake hitimisho la fungu, ambalo tunaamini kwamba Mungu atatupatia.

> *Hata alipokuwa . . . akitoka kwenda njiani, mtu mmoja akaja mbio,* akampigia magoti, . . . akamwuliza, *Mwalimu mwema, nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele?*
>
> . . . *Yesu akamwambia, Kwa nini kuniita mwema? Hakuna aliye mwema ila—ila mmoja, ndiye Mungu.*
>
> *Wazijua amri, Usizini, Usiue, Usiibe, Usishuhudie uongo, Usidanganye, Waheshimu baba yako na mama* yako.
>
> *Akajibu akamwambia, Mwalimu, haya yote nimeyashika tangu utoto wangu.*

*Yesu akamkazia macho, akampenda, akamwambia, Umepungukiwa na neno moja: enenda, ukauze ulivyo navyo vyote, uwape maskini, nawe utakuwa na* hazina *mbinguni; kisha njoo, uchukue msalaba wako, unifuate.*

*Walakini yeye akakunja uso kwa neno* hilo*, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi.*

40 Ninataka mwone kijana huyu, kwamba yeye hakuwa kafiri. Alitegemewa kuwa ni mwaminio. Alikuwa mshiriki wa kanisa. Na ningependa kuzungumza asubuhi ya leo, kwa dakika chache zijazo, sijui tu kuwa hii imetengewa muda gani, bali ningetaka kuwazungumzia juu ya Maandiko machache niliyoandika hapa chini juu ya somo la: *Uwekezaji*.

41 Ningeamini kwamba mfanyabiashara yeyote anapaswa kuvutiwa na uwekezaji mzuri. Na sisi tunazungumzia, nadhani, wafanyabiashara wa mji huu mkubwa, maarufu, New York. Na mtu yeyote anayeweza kufanya uwekezaji utakaomsaidia, anapaswa kuvutiwa na huo. Sasa tuna kila namna ya vitega uchumi. Lakini kitega uchumi ninachouliza habari zake asubuhi ya leo... Huenda ukawa na vingi vizuri, lakini hiki ndicho bora kuliko vyote uwezacho kuwekeza. Mimi, kama tu nilivyotaja, mimi ni wakala kwa ajili ya Uzima wa Milele.

42 Si biashara nzuri kucheza kamari, kubahatisha. Ninii... ndugu yetu hapa alikuwa tu akizungumza dakika chache zilizopita, juu ya, yeye alikuwa anaenda katika sehemu hizo na kucheza kamari. Huko, huko ni kubahatisha. Mfanya biashara mwenye hekima hatafanya hivyo. Hapaswi kufanya hivyo, hata hivyo. Ni kubahatisha. Wewe—wewe ungeweza kufilisika, mara moja, kwa ki—kitu kama hicho.

43 Na halafu mfanyabiashara mzuri aliye timamu, ama mfanyabiashara mzuri mwenye mawazo ya busara, asingeweza kuwekeza katika "tajirika upesi," kampuni fulani isiyojulikana, kuwekeza. Yeye, asingeweza kufanya hivyo, mfanyabiashara mzuri mwenye mawazo ya busara, kama ninavyoamini mlivyo, na wanawake.

44 Hii "tajirika upesi." Nilikuwa na rafiki wakati mmoja aliyekuwa na hazina yake ya maisha katika benki, akipata riba kidogo, ndipo mtu fulani akaja na njia ya mkato. Unajua, tunasikia leo kuhusu nyingi sana, njia za mkato ndilo jambo. Ulimwengu umejaa hizo; matangazo ya biashara, na televisheni, redio, magazeti. Na ikiwa watu wa Marekani wanaangukia kitu kama hicho!

45 Hapa muda mrefu uliopita, nilikuwa nikisikiliza tangazo la biashara kuhusu mwa—mwa—mwanamke, ama akiongea kwenye—kwenye redio. Nilikuwa kwenye motokaa yangu, nikienda mahali fulani, na wao wakasema, "Tumia sabuni hizi nzuri za unga za kuoshea vyombo" ya namna fulani, "hata haikubidi kuosha sahani. Unazitia tu humo, na kumimina

kidogo na kutikisa juu-chini; na hakuna kuosha, hakuna kusuuza, hakuna kukausha, hakuna chochote." Na ilikuwa ni mojawapo ya vitu vikuu kuliko vyote ambavyo sayansi iliwahi kutupatia.

46 Na kurudi moja kwa moja, yapata tangazo la biashara lililofuata, lilikuwa, "Usitumie hizi sabuni mpya za unga. Angalia mikono ya mama, jinsi ilivyo ya kupendeza. Hizo huichoma mikono yako. Kuwa . . . kuwa na mikono inayopendeza kama ya mama, basi usitumie sabuni mpya ya unga."

47 Na ilitokea kwamba nilikuwa naishi Jeffersonville, kwenye wakati huo, ilipo kampuni kubwa ya Colgate Palmolive Peet, na kampuni iyo hiyo ilitengeneza bidhaa zote mbili. Unaona? Unaona? Ni—ni kiinimacho. Na kuna nyingi sana za hizo ulimwenguni leo!

48 Nami ninasema hili kwa kicho na heshima, na ninatumaini halisikiki la kukufuru, bali kitu hicho hicho kimeingia katika huduma ya kanisa. Mungu hana njia za mkato. Unalipa tu gharama. Unakuja na kuchukua njia ambayo Mungu alitoa kwa ajili yetu.

49 "Tajirika upesi," unawekeza ndani yake, na, muda si muda wajua, jamaa huyu alipoteza kila kitu alichokuwa nacho. Ni biashara mbaya kufanya chochote kama hicho. Haionyeshi akili nzuri au mawazo mazuri ya biashara, katika biashara fulani isiyotambulishwa.

50 Na halafu si biashara nzuri kuweka kile ulicho nacho, mfukoni mwako, kwa sababu afadhali ukiweke katika matumizi. Unakumbuka Bwana wetu akizungumza kuhusu hizo talanta?

51 Sitakuwa na wakati wa kuchambua hili lote, bali ninatumai mnaelewa kile ni—ninachosema, nikitoa mfano hapa, kueleza jambo ambalo ninataka kuwaelezea.

52 Sasa tunakuta kwamba, ukiweka pesa zako mfukoni mwako, wezi wanaweza kuzichukua. Na sisi hatutaki kufanya hivyo, kwa sababu hiyo si sera nzuri, kuweka pesa zako mfukoni mwako. Unaweza kuzipoteza, na ungeweza, mtu fulani angeweza kuzichukua kutoka kwako.

53 Pia usiziingize katika uwekezaji fulani wa kijinga. Lakini wekeza katika kampuni fulani nzuri ya kutegemewa ambayo imethibitishwa na kutambulishwa kabisa kwamba italipa. Sasa hilo ndilo nyinyi watu hufikiria, nyinyi wanaume na wanawake wafanyabiashara. Kama hailipi, basi unaiogopa. Lakini ikiwa imethibitishwa kwamba inalipa, na ni ya kutegemewa, basi unawekeza hapo. Unaweza kuweka yote uliyo nayo katika hiyo, kwa sababu imethibitishwa, imethibitishwa kabisa, kwamba inalipa.

54 Basi mtawala huyu kijana, au mfanyabiashara kijana, ninaenda kumwita hivyo. Huyu kijana mfanyabiashara wa

mjini alikuwa na nafasi kuwekeza katika mojawapo ya mambo makubwa sana yaliyotambulishwa ulimwenguni. Alikuwa na nafasi kuchukua ha—hati ya mkataba, kama ambavyo tungeiita, ya Uzima wa Milele. Lakini hakuvutiwa na hati ya mkataba kama hiyo, kwa sababu gharama yake ilionekana kuondolea mbali mambo ya ulimwengu aliyotaka kufanya. Hiyo hapo hoja.

55 Sasa, kijana huyu alijua kwamba kulikuwa na kitu alichokuwa amepungukiwa nacho. Ingawa sisi (yeye) tunaelewa kikamilifu kwamba hapana shaka yeye alikuwa na ba—baba mzuri, mama mzuri, na ujuzi wa kanisa, kwamba alikuwa ni mshiriki wa kanisa, kwa sababu Yesu alimwuliza, "Zishike Amri. Mheshimu baba na mama. Usiue, kuzini," na maadili haya yote ambayo kanisa hufundisha. Bali hata hivyo Yesu alimwambia, "Ungali umepungukiwa kitu kimoja."

56 Yeye hakuwa, hakumwuliza Yesu, "Nifanye nini ili niweze kujiunga na kanisa Lako? Ni nini ninaweza kufanya, ili niweze kuwa m—mshiriki?" Bali alisema, "Nifanye nini kuwa na Uzima wa Milele?" Hata hivyo, akiwa ni mfuasi wa kundi la kidini, hata hivyo kijana huyo alikuwa na akili ya kutosha kujua kwamba hakuwa na Uzima wa Milele.

57 Na kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele. Tunapambana kwa ajili ya huo. Na yeye alipewa nafasi hiyo kuupokea Huo, wakati alipouliza, kwa sababu imeandikwa, "Ombeni nanyi mtapokea."

58 Basi Huo ulitolewa kwake, bali hata hivyo mpumbavu vya kutosha kukataa kwa sababu gharama ilikuwa kubwa sana. Basi kama Mkristo, na kusafiri ulimwenguni, ninakuta shauku iyo hiyo katika mioyo ya watu wengi sana leo hii. Kama mke wangu alivyozoea kusema, "Unataka kula keki yako, na kuiweka, pia." Hu—huwezi kufanya hivyo.

59 Huwezi kushikilia upendo wa ulimwengu, na kwa Mungu, wakati uo huo. "Kwa kuwa huwezi kumpenda Mungu, na mali," ambayo inamaanisha, "ulimwengu. Na kama unapenda ulimwengu, au vitu vya ulimwengu, upendo wa Baba haumo ndani yako."

60 Lakini watu wengi sana wanapenda kusema, "Mimi ni mfuasi wa *fulani*." Bali hilo silo swali. Hiyo siyo hati ya mkataba ninayozungumzia, asubuhi ya leo.

61 Ni Uzima wa Milele, Uzima usio na mwisho! Na kitu chochote kilicho cha Milele, hakikuwahi kuanza, kwa hiyo hakiwezi kuisha. Milele kamwe haianzi. Na halafu njia ya pekee uwezayo kuwa wa Milele, ni kupokea Uzima wa Milele. Na kuna kitu kimoja tu cha Milele, na hicho ni Mungu. Si kwa kujiunga na kanisa, au kanuni za imani, au kufungua ukurasa mpya kwenye Mwaka Mpya, au chochote kile; bali ni kumpokea Mungu, Utu wa Mungu, katika umbo la Roho Mtakatifu, ndani ya maisha yako. Na unakuwa sehemu ya Mungu, na wa Milele tu kama

Yeye alivyo, kwa sababu wewe ni sehemu Yake. Kila kitu kilicho na mwanzo kina mwisho. Ulimwengu ulianza, unaisha; mbingu inaanza, inaisha. Yesu alisema, “Mbingu na nchi zitapita, bali Maneno Yangu hayatapita,” kwa sababu Yeye ni Neno. Yeye ni Neno, na hilo ni la Milele.

62 Basi Neno hilo ndani yako huzaa Uhai wa Kristo. Kama ningeweza kuchukua uhai kutoka kwa mpichi na kuuweka ndani ya mpea, usingezaa pichi tena, ungekuwa na pea juu yake kwa sababu uhai ulio katika mti utazaa kile ulicho. Uhai ulioko ndani yako huonyesha kile ulicho. Maisha yako yanashuhudia kwa sauti kubwa mno, ndani yako, mpaka ushuhuda wako hausikiki. Wanajua kile ulicho kwa maisha unayoishi na mambo unayofanya. Kama uhai wa Kristo uko ndani yako, basi, hivyo basi, kazi na Maisha ya Kristo unaishi, kwa sababu huo ni Uhai Wake ukiishi kupitia kwako. Uko tu katika chombo kuendeleza kazi ya Mungu.

63 Ni kitu cha kijinga jinsi gani alichofanya kijana huyu wakati yeye—yeye hakuvutiwa na uwekezaji wa namna hiyo. Alikuwa na mali nyingi, tunaambiwa. Lakini mali ya ulimwengu haina budi kuangamia. Vipi kuhusu hali ya kijana huyo leo hii, unashangaa mahali alipo? Alikataa fursa aliyokuwa nayo. Hata hivyo, alikuwa ni Mkristo mwaminio, ama mwaminio, tungesema, kuwa wa kimsingi zaidi. Alikuwa ni mwaminio, alikuwa anatembea katika nuru yote ambayo torati ilikuwa nayo, na labda mshiriki mwaminifu wa kusanyiko fulani kubwa, lakini hata hivyo alijua kwamba alipungukiwa Uzima wa Milele.

64 Sasa, alikuwa ameona kitu fulani ndani ya Yesu ambacho hakuwahi kuona ndani ya watu wengine. Alikuwa ameona makuhani wake, akaona watu wake, alikuwa ameona watu wema, bali kulikuwa na kitu maalum kuhusu Yesu Kristo. Waliona, hata waandishi na askari wa vita waliotumwa, na kutoka hekaluni, kumkamata Yeye, walisema, “Hakuna mtu aliyewahi kunena namna hii.” Si tu kwamba alinena kama kuhani au m—mlei, bali Yeye—Yeye alikuwa . . . Mungu aliunga mkono kile Yeye alichosema. Yeye alikuwa . . .

65 Hakuandika vitabu vyovyote. Hatuna chochote ambacho Yesu aliwahi kuandika, maishani Mwake. Jambo pekee tujualo, Yeye aliandika wakati mmoja juu ya mchanga, wakati ma—maskini mama fulani katika sifa mbaya aliletwa Kwake, ndipo Yeye alifuta hayo kabisa. Ni kwa nini Yeye hakuandika? Yeye alikuwa ni Neno. Alikuwa ndiye thibitisho lililo hai kwamba kuna Mungu aishiye, Uhai Wake wenyewe ndani Yake.

66 Alisema, “Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Ijapokuwa hamwezi kuniamini Mimi,” maana Yeye akiwa ni mwanadamu, “hata hivyo aminini kazi. Yachunguzeni Maandiko, maana ndani ya Hayo mnadhani

mna Uzima wa Milele, na Hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Yanawaambieni kuwa mimi ni Nani." Hiyo ilikuwa lugha ngeni kwa wengi wa hao makasisi wa siku hiyo.

67 Ni vibaya sana, inaonekana kuwa inajirudia tena. Lakini, ni kwamba, ulimwengu unabakia vile vile. Roho hazibadiliki, hutoka kwa kundi moja hadi jingine, mtu mmoja hadi mwingine; roho waovu, na Roho mzuri kutoka kwa Mungu. Roho Mtakatifu hubakia vile vile kama Yeye alivyokuwa wakati Yeye aliposhuka upya kwenye Siku ya Pentekoste, wakati Mungu, katika ile Nguzo kuu ya Moto, alipojigawa Mwenyewe miongoni mwa watu Wake.

68 Lakini katika huyu Yesu, aliona kitu ambacho hakuna mtu mwingine alikuwa nacho, alimwona Mungu akiishi ndani ya mwanadamu.

69 Ndipo basi, kama watu werevu wenye mawazo, asubuhi ya leo, kama Uhai ule ule uliokuwa ndani ya Kristo uko ndani yako, Huo unawezaje kukosa kuishi kitu kile kile, na kuwa kitu kile kile? Hauna budi kufanya hivyo. Kwa hiyo huenda tukachochewa kwa njia ya msisimko, huenda tukajazwa kasumba na kanuni fulani ya imani au kitu fulani, hata tungeweza kufikiria hicho kilikuwa ndicho. Lakini wakati tunaposoma kile Yeye alichokuwa, basi hicho ndicho Yeye alicho leo hii. Kile ambacho Mungu alikuwa ndani ya Kristo, Ndugu yenu Mkombozi, hicho ndicho Yeye alicho ndani yako kama mtoto aliyekombolewa.

70 Yesu alimwona huyu kijana mwanamume, na Yeye akampenda. Sasa kuna kitu kimoja ambacho tunaonekana kupungukiwa nacho kwa wingi, leo, kwa sababu watu ambao hawatupendi, inaonekana kama hatutaki kuwapenda. Tangu nimekuwa miongoni mwa watu wa Full Gospel, na hilo ni jambo moja ninalopata, hadi nilipokutana na kundi hili la Wafanyabiashara, kwamba madhehebu ya imani za Kipentekoste yanaonekana kujitenga yenyewe. Huko si kudhihirisha Maisha ya Yesu Kristo. Yeye alipenda wote, na Yeye alimpenda huyu mfanyabiashara kijana. Ingawa alimkataa Yeye, hata hivyo Yeye alimpenda.

71 Na kijana huyu alipata kitu fulani ndani ya Yesu ambacho hakupata mahali popote pengine, na alialikwa kupokea hiki ambacho Yeye alikuwa nacho, bali gharama ilikuwa kubwa kupita kiasi. Na ingawa alikuwa ameona kwamba kitega uchumi alichokuwa ameulizwa kuwekezea, kilimgharimu mali yake yote ya duniani, kwa kuwa Yesu alimwambia, "Nenda ukauze ulicho nacho."

72 Sasa, wanaume na wanawake, msi—msinielewe vibaya. Simaanishi haitupasi kuwa na pesa. Lakini ukiifanya hiyo kuwa Mungu wako, wakati hiyo ndiyo unayotegemea, haina budi kuangamia. Basi leo hii, mara nyingi sana, ambapo wanaume na wanawake wafanyabiashara wanajaribu kuona ni kiasi gani

wanachoweza kupata, ambapo tunapaswa kuwa tukiona ni kiasi gani tunaweza kuachilia. Jinsi ilivyo tofauti leo hii, katika milki za Kikristo, na katika makanisa ya kimadhehebu, na kadhalika, yote hayo. Ni tofauti kiasi gani inavyoonekana kuwa, leo hii, kuliko kanisa la Pentekoste la mwanzoni. Leo hii wanaonekana kujaribu kujivuna juu ya, "Nina mlolongo wa Kadilaki, na mimi ni wa kiroho kwa sababu nina mali nyingi sana za ulimwenguni." Na tunaona hicho kimetukuzwa kupita kiasi, hata miongoni mwa ndugu zetu. Pentekoste ya siku za mwanzoni waliuza walichokuwa nacho na kuwagawia maskini, na miongoni mwao.

73 Kijana mmoja si muda mrefu uliopita, huko Jamaica, ambapo tulikuwa kwenye uwanja wa mashindano ya riadha, nilikuwa pamoja na Wafanyabiashara wa Full Gospel. Nilitoa tamshi kitu kama hicho, usiku mmoja, kwa mkutano wa wafanyabiashara waliokuwa wamekusanyika kutoka kote visiwani, chini kote—kote visiwani. Ndipo mwimbaji huyu kijana akanijia, na akasema, "Ndugu Branham, tamshi lako halikuwa mashuhuri sana, usiku wa leo, juu ya kile ulichosema kuhusu wapentekoste kuuza walichokuwa nacho."

74 Nilikuwa nikihubiri juu ya wakosoaji wa pentekoste, na kusema kwamba hapo ndipo walipokuwa na haki kukosoa kitu hicho kimoja. Nikasema, "Nyinyi wafanyabiashara daima mnaeleza jinsi ya kuwa tajiri. Watu hao wanajua jinsi ya kuwa tajiri. Ni matajiri tayari. Kitu unachotakiwa kuwauzia ni Yesu Kristo, kitu ambacho hawana."

75 Huwezi kuipeleka Injili huko ulimwenguni. Inatubidi kuuleta ulimwengu hapa. Hollywood hufuata vitu vinavyometameta, tumbili hufanya jambo lilo hilo. Hollywood hung'aa, bali Injili humeka. Kuna tofauti kubwa kati ya kung'aa na kumeka. Tunajaribu kuvaa vitu vikubwa, na kuwa kitu fulani kikubwa. Hiyo siyo njia ya kumpata aliye nje. Ishi Maisha, na umruhusu Kristo aishi ndani yako, hiyo humfanya kuwa na njaa na kiu kuwa kama wewe. Unapokolea chumvi, yeye ataona kiu. Njia ya pekee unayoweza kukolea chumvi ni kuruhusu Uhai wa Kristo uwe ndani yako, kwa kuwa Yeye ni huo. Chumvi huokoa tu inapogusa.

76 Sasa tunaona, kijana huyu mwanaume alijua kwamba Mtu huyu alikuwa ni zaidi ya mwanadamu tu wa kawaida. Alijua Yeye hana budi kuwa ni Mungu, kwa sababu Uhai wa Mungu ulikuwa ukiakisi kupitia Yeye; na Yeye alithibitishwa kikamilifu na Neno, kwamba Yeye alikuwa Mungu.

77 Sasa ninataka kuzungumza kwa muda mfupi tu kwa ndugu zangu wahudumu, pia. Sisi ni kusanyiko hapa la wahudumu na wafanyabishara pia. Ninahofia tu kidogo kwamba mfumo wetu mkubwa wa makanisa yetu leo hii umefikia mahali hapo, kwa kuwa Biblia inadai kwamba tutafika, katika siku za mwisho, kwenye Wakati wa Kanisa la Laodikia, "ambao ni 'tajiri, una

mali, hauna haja ya chochote.' Nawe hujui kwamba wewe ni mwenye mashaka, maskini, mnyonge, kipofu, nawe hujui." Hiyo ndiyo sehemu yenye huzuni, "Hujui! Umepofushwa!"

78 Ni kwa nini hao Mafarisayo, wasomi wa seminari wasingeweza kumjua Yesu Kristo, wakati Yeye alitambulishwa kikamilifu na Biblia, wakati Yeye alithibitisha kwamba Yeye alikuwa ndiye Nabii ambaye Musa alisema atainuliwa? Na wao hawakuwa na manabii kwa mamia ya miaka. Na hapa Yeye alisimama miongoni mwao, akiwa na Neno hasa la Mungu, bali Biblia ilisema kwamba wao walikuwa "Mafarisayo vipofu." Pia Biblia inatwambia, kwamba, "Hawana budi kuwa vipofu." Ni kitu cha kusikitisha jinsi gani!

79 Nayo Biblia iyo hiyo iliyosema kwamba wangekuwa vipofu, ilisema, "Wakati wa Kanisa la Laodikia utakuwa kipofu, mwenye mashaka, mnyonge, maskini, uchi, na kipofu, wala hawajui."

80 Kama tungempata mtu mtaani, au mtu ambaye alikuwa katika hali hiyo, lingekuwa ni jambo la kusikitisha; kama ungeweza kumwendea sasa, na kuzungumza na yeye mwanamume au mwanamke. Na kama ungeangalia mavazi ya baadhi ya wanawake wetu wa kisasa, utagundua kwamba karibu wako hivyo katika njia ya kimwili. Lakini ukiwaendea na kuwaambia kwamba wamekosea, na kama wangesikiliza, waelewe kwamba wako uchi, wangejaribu kujisaidia. Bali, "Uchi, wala hawajui."

81 Sasa katika siku hii, Mungu ametuma Roho Mtakatifu kurudi, ambaye, kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele, basi Yeye angali ni Masihi yule yule. Na Uhai wa Kristo umo katika Kanisa Lake, ukithibitisha Neno Lake. Hivyo ndivyo Mungu alivyokuwa duniani, katika mwili wa Yesu Kristo, akiwa ni Neno, kufanya Neno kuishi. Na Roho Mtakatifu leo yuko katika mwili, akilifanya Neno la Mungu liishi kwa kila ahadi na kila ajabu. Na kila kitu ambacho Yeye aliahidi, kipo.

82 Nayo makanisa yamepewa nafasi ya kupokea hati hii ya mkataba wa Uzima wa Milele, lakini yalifanya kosa la kijinga ambalo yule mtawala kijana alifanya. Wameenda nje kwenye mabaraza, yakiunganika pamoja, yote yakija chini ya namna ya uongozi wa kidini ambao umetabiriwa na Biblia. Tunaona hilo katika mifumo yetu ya kimadhehebu. Na hayo yako Rumi, na kadhalika, sasa. Sasa hatuna mashoka ya kunoa, hakuna mashambulizi ya kufanya, sema tu Kweli. Hivyo ndivyo ilivyoandikwa. Mungu daima huthibitisha kweli Yake. Nalo kanisa katika hali kama hiyo, imepewa nafasi kuchukua Hati ya mkataba.

83 Na juu ya msingi uo huo, ambao wengi wenu wafanyabiashara hapa asubuhi ya leo, mkiwa wafuasi wa makanisa hayo. Sisemi, "Achana nayo." La, bwana. Wewe nenda

huko na uwe nuru, lakini uichukue Nuru pamoja nawe. Unaona? Angalia.

84 Msingi ule ule ambao yule mtawala tajiri kijana aliikataa fursa, msingi uo huo ni kwamba kanisa linakataa fursa leo hii kwa ajili ya Uzima wa Milele. Kwa sababu kanisa lenyewe, ingechafua urithi wao wa baba zao, mapokeo makubwa ambayo baba zao walisimamia. Na halafu ikiwa Roho Mtakatifu alishuka katika mfumo fulani mkubwa wa kidini, mbona, ninahofia kwamba maofisa hawatachukuliana naye. Angefukuzwa kutoka kwa dhehebu hilo. Unaona? Na ni vigumu kwao kumudu kufanya hivyo, asingekuwa tena "daktari, baba mtakatifu," chochote kilichokuwa, angekuwa tu mtu wa kawaida miongoni mwetu.

85 Hakuna watu wakubwa katika Ukristo. Huo ni ulimwengu unaofanya hivyo. Sisi sote ni saizi moja, wana na binti za Mungu, na si yeyote "mtakatifu kukuliko." Sisi ni watoto wa Mungu, kwa neema ya Mungu.

86 Nilisoma katika Biblia, kwamba Mungu alimwambia Yohana, kwenye Kisiwa cha Patimo, kwamba, "matendo ya Wanikolao," Yeye aliyachukia. *Nikao,* "teka walei," kuwateka walei na kuweka utakatifu wote katika watu fulani. Utakatifu ni kwa wote. Roho Mtakatifu alishuka juu ya kundi lote. Hakuna mtu mtakatifu, hata hivyo, ni Mungu mtakatifu. Hatusemi "kanisa takatifu, watu watakatifu." Ni "Mungu mtakatifu." Sisi si watakatifu, bali Yeye ni mtakatifu. Si mhudumu mtakatifu; ni Roho Mtakatifu, Yeye anahudumu kupitia mhudumu. Si watu watakatifu; sisi hakuna mmoja wetu aliye mtakatifu. Lakini wao inavyoonekana, mara nyingi sana, wanakataa fursa iyo hiyo.

87 Katika Ufunuo 3, tunasoma hili, kwamba Kanisa la Laodikia, tumechorwa mojawapo ya picha zenye huzuni kuliko picha zote za Biblia nzima, Ufunuo 3, kwenye Kanisa la Laodikia. Makanisa mengine yote, kupitia Wakati wa Luther, na Nyakati Saba za Kanisa, kila mmoja, haikuninii, kasema kuhusu Yesu kuwa ndani ya kanisa, "Yeye aliye ndani ya kanisa." Lakini katika Laodikia, Yeye alikuwa nje, akibisha, akijaribu kurudi ndani. Ni kitu cha kusikitisha namna gani kuwazia, kwamba, "Mwana wa Mungu, akibisha katika kanisa Lake Mwenyewe, akijaribu kurudi ndani."

88 Lakini utajiri wa ulimwengu huu umepofusha macho yao. Si tu tajiri wa pesa, bali tajiri katika umaarufu, tajiri katika mambo ya ulimwengu, mahangaiko ya maisha, mpaka mmechangamana, na watu wenye elimu wameingia ndani na kuondolea mbali hiyo Punje, ile—ile Lulu yenye thamani kubwa. Lakini Mungu aliwachagua watu kimbele kuwa huko; mtu fulani anaenda kuwepo huko. Bali wao wanaikataa Hiyo. Si wote watakaofanya hivyo; baadhi yao wataipokea Hiyo. Sasa

walimweka nje ya upendo wao, upendo wao wa Neno Lake. Ninii . . . Wanachukua kanuni ya imani na kuiingiza hiyo kanuni ya imani, chochote unachochukua badala ya kitu fulani.

89 Kwa mfano, ulimwoa mwanamke mzuri. Alikupenda na wewe ulimpenda, ulisema. Baada ya kitambo, ukimchukua mwanamke mwingine, au ukichukua mwanamume mwingine, inakubidi kukataa upendo wako wa kwanza.

90 Na hiyo ndiyo njia pekee tunaweza kuingiza kanuni ya imani, ni wakati tukikataa upendo wetu wa kwanza, Neno. Huwezi kuamini kosa, mpaka kwanza uikanyage Kweli. Lakini tumefikia mahali mpaka tunapeana mikono, na kuwaweka kanisani. Wangali wanavuta sigara, kunywa pombe, kufanya karamu.

91 Nilikuwa nikizungumza jana usiku, nikiteremka kwenye lifti. Kulikuwa na mama fulani kwenye lifti, akizungumzia kuhusu kuwa alikuwa anaenda kwenye karamu ya kanisa, kasema, "Iko kwenye orofa ya chini ya kanisa. Tunaenda kucheza kamari, na walikuwa na mabata bukini waliokuwa wanaenda kutoa, na hii ilikuwa ni kusaidia kulipa mchungaji na umishenari." Unaona, unaingiza kitu fulani. Huo sio mpango wa Mungu. Ikifikia mahali ambapo siwezi kuhubiri Injili, mpaka ni kujihusisha katika mambo kama hayo, ningefunga Biblia na kuenda nyumbani. Ni vibaya sana. Lakini tunayo (kwa nini?) kwa sababu imekataa hati ya mkataba ya Uzima wa Milele. Hilo ndilo hufanya hili, wamepoteza upendo wao.

92 Niliingia mahali padogo katika ukumbi wa hotelini, usiku kabla ya jana, na nilikuwa ninaenda kula sandwichi, ndipo nikamwambia mama huyo, "Niletee sa—sandwichi na bilauri ya mtindi wa maziwa."

93 Na mimi sina hakika kama nimesema hili vizuri, au sivyo. Lakini maskini mama huyo alionekana kama alikuwa ameoza, akiwa na hiyo samawati yote chini ya macho yake na kadhalika; na—na amevaa nguo za kutosha karibu, ungeweza kuweka kwenye katoni ya asprini. Akasema, "Unataka bourbon kavu?"

Nikasema, "Samahani?"

Akasema, "Bourbon nini?"

Nikasema, "Nilisema 'mtindi wa maziwa.'" Unaona?

Akasema, "Vema, unataka kunywa nini?"

Nikasema, "Mtindi wa maziwa."

Akasema, "Vema, tuna vinywaji vizuri vilivyochanganywa hapa."

Nikasema, "Mama, mimi ni mhudumu wa Injili."

94 Akasema, "Nanii wetu . . . Mimi ni Mkatoliki." Tena akasema, "Makasisi wetu huja na kunywa pombe."

95 Nikasema, "Mimi—mimi si kasisi wa Katoliki. Mimi ni mhudumu wa Injili."

Akasema, "Hivi hutakunywa kinywaji kilichochanganywa?"

96 Nikasema, "Usichanyanye huo na chochote, niletee tu mtindi wa maziwa pekee." Naam. Na yeye hakujua. Lakini wewe hapo, unaona, wewe hapo.

97 Dini, sawa tu na ulimwengu. *Dini* maana yake "kifuniko." Kama unaweza kufunikwa na ulimwengu, utatenda kama ulimwengu.

98 Bali ukiwa umefunikwa na Damu ya Yesu Kristo, uliunganishwa na Yeye, hujali mambo hayo tena. Huoni chochote ila Damu. Na Mungu hutambua Damu pekee. "Nionapo Damu, nitapita juu yako." Amina. Tunamshukuru Mungu kwa ajili ya mambo haya.

Sasa tunazungumza kuhusu hati hii ya mkataba wa Uzima wa Milele.

99 Na mara nyingi, kwa kuwa miongoni mwa watu hao Wapentekoste, wao—wao wanaweza tu kuhubiri upesi sana, na, na mimi—mimi—mimi ni mwenda pole sana. Mimi ni—mimi ni mwasi, kwa kuanzia, Mkusini; i—inanibidi tu kuchukua muda wangu. Kama hapa nje mtaani, karibu wanikanyage, ndipo mimi—mimi ninarudi nyuma kwenye kona, na kungojea mpaka umati wote upite. Na ndipo inaonekana kama haikomei hapa, kwa hiyo kwa namna fulani mimi ni mwenda pole, inawabidi kunivumilia kidogo.

100 Hebu tuwazie ba—baadhi ya wamiliki wa hati hii ya mkataba. Hebu tuwekeze hii, tuchunguze, hasa, asubuhi ya leo, baadhi ya watu ambao wamechukua hati hii ya mkataba, hapo kabla, kusudi tuweze kuona kama hati hii ya mkataba ni ya kutegemewa, au sivyo. Ninazungumza kuhusu Neno la Mungu, ambalo ni Kristo katika mwili. Mtu fulani ambaye ameshikilia hati hii ya mkataba, tutaanzia huko nyuma na upesi kupitia wamiliki wachache.

101 Kulikuwa na mtu, wakati mmoja, aliyepewa hati hii ya mkataba. Alikuwa ni mkulima. Na Bwana Mungu akakutana naye na Neno Lake, na kusema, "Kunaenda kuwa na gha—gharika ambayo inaenda kuangamiza ulimwengu mzima. Wewe unaenda kutenda kiajabu sana sasa kama unataka kupokea hati hii ya mkataba, bali itaokoa maisha yako. Ninataka ujenge safina." Alikuwa ni Nuhu. Na ingawa ulimwengu wote wa kidini, katika siku hiyo, ulidhania mzee huyo alikuwa mwendawazimu, na hakika haikulingana na utaratibu wa kisayansi wa siku hiyo.

102 Kwa sababu, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu," ulimwengu kama huo, "ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu," wakati hati ya mkataba ina majina mengi sana yaliyoandikwa juu yake; na Yeye yuko kule

juu, akikomboa, asubuhi ya leo, wale wote ambao watakuwa na jina lao katika Kitabu hicho. Sasa, baada ya kitambo, jina la mwisho linaingia, na hilo ni . . . Hilo litaimaliza. Ingieni sasa, ndugu zangu. Msingoje. Baada ya kitambo, huenda ikachelewa sana. Njoo sasa wakati ukiwa na nafasi, wakati wewe . . . wakati imetolewa kwako.

103 Tunaona kwamba Nuhu alifanya uwekezaji huu, alikuwa mkulima mashuhuri sana, na labda aliwajua watu wengi, na alikuwa na vitu vikubwa. Lakini aliuza, labda shamba lake, kupata vifaa vya kujenga safina. Watu walimcheka; Shetani alisababisha hayo. Huenda aliitwa "mtakatifu anayejibingirisha."

104 Kama mmoja alivyosema asubuhi ya leo, alifanyika mtakatifu wa kubingirika sakafuni, wakati alipopata na kutia sahihi jina lake katika Damu ya Bwana Yesu, kwamba alitaka kumiliki hati hii ya mkataba.

105 Na yeye, Nuhu, alifanya jambo lile lile. Na alitoa kile alichokuwa nacho, ndipo akajenga safina. Alichekwa, akajaribiwa na Shetani, lakini tunapata kwamba hati yake ya mkataba ililipa katika kuokoa maisha yake; siyo tu maisha yake, bali nyumba yake.

106 Na mimi ninaamini kwamba hiyo ni kweli. Si wewe pekee; labda m—mke, mwanamke mfanyabiashara, mwanaume, mfanyabiashara.

Unasema, "Hiyo ina uhusiano gani na familia yangu?"

107 Liliulizwa wakati mmoja, Paulo na Sila. Mlinzi wa gereza Mfilipi, alisema, "Nifanye nini ili nipate Uzima wa Milele?"

108 Akasema, "Mwamini Bwana Yesu Kristo, na wewe na nyumba yako!" Kwa nini? Kama yeye kwa kweli, si imani ya kujifanya, bali aamini! Yesu alisema, "Ishara hizi," katika Marko 16, "zitafuatana," si labda, "zitafuatana na hao waaminio." Na kama una imani ya kutosha kwa wokovu wako mwenyewe, unaweza pia kuidai familia yako mwenyewe, kwa imani. Ikiwa una imani ya namna hiyo, imani yako inaweza kusaidia familia yako, "wewe na nyumba yako."

109 Na familia ya Nuhu, wakiona kwamba baba yao, mtu mwema, alikuwa akitwanga, wana wake na wake wa wanawe, na kadhalika, walikuja kutwanga pamoja naye, wakibeba shutuma la Neno. Daima inakubidi kufanya hivyo. Ufalme wa Mungu hauji bila ya majaribu. Watu hujisukumiza ndani Yake, ndani ya Ufalme wa Mungu; si kuchunguza. Sasa, lakini ililipa, katika kuokoa maisha yake. Tungeweza kukaa saa nyingi juu ya Nuhu.

110 Lakini hebu tuende kwa mwingine, jina lake Danieli. Akiwa nabii, majaliwa yalifanyika nabii wa Mungu. Nalo Neno la Mungu humjia nabii pekee. Hakuna njia nyingine. Daima humjia nabii.

111 Sh, hebu kidogo. [Ndugu fulani anaongea katika lugha nyingine. Ndugu mmoja anatoa tafsiri—Mh.] Amina. Mshukuru Bwana. Tunaelewa. Labda kwa wale ambao wasingeelewa, mfanyabiashara, ni—nisingesema chochote cha kukosoa kuhusu hilo. Unaona, halina budi kuwa jambo muhimu, kwamba Roho Mtakatifu angekatiza juu ya Ujumbe, kufanya jambo kama hilo, kutoa onyo.

112 Sasa tunaamini lugha zisizojulikana, kama karama. Nilizoea kuwazia kwamba ilikuwa ni kosa. Wakati nilipokuwa tu nimekuja kwa mara ya kwanza miongoni mwa watu, nilifikiria kwamba labda watu hao, wanaonena katika lugha, labda walikuwa wanajiwekelea tu hilo. Lakini nisingeweza kusema chochote, kwa sababu, kumbukeni, tunaweza kumkufuru Roho Mtakatifu, yaani, kuzungumza kuhusu kitu kibaya. Kwa hiyo ninakuta, nilipoenda Afrika na kusafiri kote ulimwenguni, hakuna sauti bila ya umuhimu wake. Kila mlio mdogo wa kuku na hatua ina maana ya aina fulani.

113 Basi tunatulia tu mpaka Roho Mtakatifu anene Neno Lake tena. Na hiyo ndiyo sababu, labda, Yeye alikatiza Ujumbe, kusema, kama nilivyoelewa, nadhani nilielewa, kwamba, "Yasikieni Maneno ya Bwana, na kutii Maneno ya Bwana." Sasa, kumbukeni tu, huyo hakuwa ni mimi. Huyo alikuwa ni watu, watu wenye vipawa, pamoja na kunena katika lugha zingine. Na—na hao watu, wenyewe, wasingeweza kufanya hivyo, sidhani. Wakati Ujumbe ulikuwa unaendelea, wasingenena, kama halikuwa ni jambo ambalo Roho Mtakatifu kwa dharura alikuwa analeta labda kwa nafsi moja hapa. Sijui. Unaona, sijui chochote kuhusu hilo, hilo ni juu ya Mungu. Unaona? Lakini sisi daima tunataka kuheshimu na kuwa na kicho kwa chochote ambacho Mungu angefanya.

114 Sasa turudi kwenye wazo la wenye hati za mkataba, wa hati ile ile ya mkataba ambayo watu hawa pia wamejazwa nayo, kufanya kazi hizi sasa, kuleta katikati ya Ujumbe, kitu cha kuingiza humo na kusema, "Huyu ni Roho Mtakatifu," maneno mengine, "anayewazungumzia."

115 Danieli, alikuwa ndiye ambaye tulikuwa tukiongea naye. . . Alikuwa mmiliki wa hati ya mkataba. Alikuwa ni mtu aliyejazwa na Roho wa Mungu. Kwa sababu Neno lilikuwa ndani ya Danieli, Danieli alikuwa nabii.

116 Nayo Biblia ilisema, katika Waebrania mlango wa kwanza, "Katika ninii. . .nyakati za kale, Mungu, kwa njia mbalimbali, sehemu nyingi, alinena na baba zetu kwa njia ya manabii." Sasa *nabii* ni neno lenye maana mbalimbali, ambalo linamaanisha "mfunuaji wa Maandiko" na "mtabiri wa mambo yanayokuja," kuonyesha kwamba Mungu habadilishi Ujumbe Wake. Kila wakati, Mungu daima ametumia, si dhehebu, wala kundi au mfumo, bali mtu.

117 Naye Mungu asiyebadilika, Yeye aliandaa njia moja katika bustani ya Edeni, ambayo watu wanapaswa kuokolewa, hiyo ni kupitia Damu. Tunaweza kuwa na mifumo ya elimu na mifumo ya kimadhehebu, bali Mungu anaikataa. Ingali inabaki Damu. Hiyo ndiyo njia pekee.

118 Mungu humtumia mtu binafsi. Watu wawili kamwe hawatakiona kitu hicho kwa njia sawa, kwa hiyo Mungu anaweza tu kumpata mtu mmoja mkononi Mwake; halafu kupitia pale, kama Musa na kupitia Danieli, na kupitia manabii mbalimbali. Pia sikilizeni.

119 Unasema, "Vema, vipi kuhusu Roho Mtakatifu?" Roho Mtakatifu habadilishi hilo.

120 Tazama, Neno la Bwana humjia nabii. Yohana alikuwa ndiye nabii wa majira hayo. Alikuwa amesimama ndani ya maji, akitangaza kwamba Masihi alikuwa tayari miongoni mwao, mahali fulani. Angelijua hilo kwa ishara. Na wakati Masihi, akiwa ni Neno, Yeye alikuja ndani ya maji, kwa nabii, Neno likimjia nabii!

121 Yesu alisema, katika siku hizi, Yeye alisema, "Yeye," ambacho ni kiwakilishi nafsi, "Yeye Roho Mtakatifu, wakati Yeye amekuja juu yako, akakujia, Yeye atawaonyesha mambo haya niliyowafundisha, na atawaonyesha mambo yajayo." Kinabaki kitu kile kile, Roho Mtakatifu ndiye Nabii miongoni mwetu leo hii. Roho Mtakatifu ndiye Nabii.

122 Danieli alikuwa nabii. Maneno ya Mungu, Biblia, ilikabidhiwa Danieli, kudhihirisha kwa watu kwamba Mungu alikuwa angali anaishi. Ndipo Danieli alikusudia moyoni mwake kwamba asingeuchafua uwekezaji wake.

123 Loo, laiti kanisa lingaliweza tu kufanya hilo, laiti kanisa lingalikusudia tu moyoni mwako kwamba hutauchafua uwekezaji wako na kujifunga kokote na mambo ambayo hukuleta katika mfumo ambao utakupeleka mbali na Yeye!

124 Danieli alikusudia moyoni mwake. Na huo ulifanya nini? Uliyaokoa maisha yake kutokana na simba.

125 Wana wa Kiebrania waliwekeza katika Mungu, kwamba wasingezivunja amri Zake, haijalishi kama walitengeneza sanamu ya ndugu yao mtakatifu, Danieli. Ambayo, ninaamini sanamu ilikuwa ya Danieli, maana yeye alikuwa ni mungu wa Belteshaza, na tunapata ya kwamba yeye alitengeneza sanamu kwa mtu huyu mtakatifu. Haijalishi jinsi mtu huyo alivyokuwa mtakatifu, hawakupaswa kusujudia sanamu ya aina yoyote, haijalishi sanamu hiyo ni kitu gani. Ulimwengu wa Mataifa uliingizwa ndani kwa kuabudu sanamu takatifu, unaondoka kwa njia iyo hiyo, na mnaona mfumo ukifanya hivyo leo hii. Kwa hiyo watoto wa Kiebrania wasingesujudia sanamu yoyote, na unapata ya kwamba uwekezaji wao ulilipa kwa kuokoa maisha yao.

126 Sasa dakika chache tu, tunamkuta jamaa mwingine jina lake. . .yeye ni mfanyabiashara wa uchumi, mfanyabiashara ambaye alikuwa na kazi ya biashara. Yeye—yeye alikuwa ni mvuvi wa samaki. Aliitwa Simoni. Naye ndugu yake alikuwa Andrea. Baba yake aliitwa Yona. La, samahani. Naam, ilikuwa. Ninaamini hiyo ni sahihi.

127 Na kwa hiyo tunaona kwamba ndugu yake huyu mvua samaki alikuwa akihudhuria uamsho wa kibaptisti, Yohana mbatizaji. Na alikuwa, huyu mbatizaji alisema, "Sijapata Hiyo, lakini Hiyo inakuja."

128 Lingekuwa ni jambo jema kama dhehebu letu, na mimi nikiwa ni Mbaptisti kwa kitambo, lingefanya jambo lilo hilo. Naam, Hiyo inakuja. Ikiwa wewe. . .Itabidi ije kutoka Juu. Ni ahadi.

129 Basi siku moja huyu mbaptisti, ama mbatizaji, alitangaza, "Ile pale, moja kwa moja miongoni mwenu."

130 Ilimfurahisha sana Andrea mpaka akaenda kumleta ndugu yake, mvuvi wa samaki.

131 Alikuwa na shughuli nyingi sana katika biashara yake, mpaka, asubuhi moja huenda alihudhuria ki—kiamshakinywa. Sijui kile alichohudhuria, ilikuwa ni chini kwenye ufuko. Na wakati alipofanya hivyo, alitembea akaingia katika Uwepo wa Mnenaji, ndipo Mnenaji akasema, "Jina lako ni Simoni, na wewe ni baba . . . Yona ndiye baba yako."

132 Upesi sana, huyo mshiriki wa Sanhedrin, huyo mshiriki wa kundi kubwa la kikasisi, ambaye alikuwa amesoma Biblia yake na kujua kwamba mtu yule yule, Musa, ambaye walikuwa wakimfuata, alikuwa amewaambia kwamba, "Ajapo Masihi, Yeye atakuwa ni Nabii." Alisikiliza kile ambacho Neno lilisema, bila kujali kile kilichokuwa mfumo wa kikasisi aliokuwa mshiriki wake.

133 Hivi sisi, leo hii, tusingeweza kumsikiliza Mtu yuyo huyo, Yesu Kristo, Yule aliyetuambia kile ambacho kingefanyika hapa katika siku za mwisho?

134 Na vile alivyomjia Mtu huyu, na Yeye akamwambia kuwa yeye alikuwa ni nani; si yeye pekee, bali maskini baba yake mtauwa aliyekuwa ameondoka; upesi aliwekeza katika hati hii ya mkataba, Uzima wa Milele, na kufanyika askofu huko Rumi, katika kanisa. Nathanaeli, baada . . .

135 Kuna mtu pale jina lake Filipo aliyekuwa ameona hayo, na ikamfurahisha sana! Alijua huyo alikuwa ni Masihi, kwa sababu Yeye alikuwa ni Nabii. Walishakuwa na kila namna ya manabii, bali haikuwa ni aina sahihi ya Nabii. Wakati walipomwona Nabii huyu akija, ametambulishwa kikamilifu na Neno!

136 Hivyo ndivyo kanisa lilivyo nabii leo hii, linapaswa kutambulishwa kikamilifu na Neno la Mungu, ambalo

ndilo Nabii. Na tukijiundia wenyewe madhehebu na kupata makundi, na kutengana mmoja na mwenzake, "bila ya Imani inavyoonekana," tunaendaje kuchukua Neno? Unaona, hatuwezi kulichukua. Rudini kwenye Neno, Hili ni Uzima wa Milele, "Maneno yangu ni Uzima."

137 Sasa angalia kilichotukia. Tunamwona Filipo akipata shauku kubwa, mpaka akakimbia kuzunguka mlima. Kama utapima: hapo, ama kuwahi kuwa huko, ni karibu maili kumi na tano. Labda alirudi siku iliyofuata, akimleta mtu, Nathanaeli; ambaye alikuwa amempata rafiki yake, ambaye walikuwa wamesoma Biblia pamoja. Na yeye alikuwa chini ya mzeituni, akiomba, kwa sababu alikuwa na kimsitu. Ndipo, upesi, kamwe hakuwa na wakati wowote sasa kujipumbaza, yeye pia alikuwa ni mmiliki wa hati ya mkataba na alikuwa anataka kuwaonyesha wengine. Wakati ukipata hati hii ya mkataba, kuna kitu kuihusu, unakuwa mwuzaji upesi sana. Na yeye kamwe hakungojea au kuzungumzia jinsi ambavyo kijisitu chake kilivyokuwa kinaendelea. Alisema, "Njoo, uone Yeye tuliyempata, Yesu mwana wa Yusufu, Yesu wa Nazareti!"

138 Upesi huyu Mwebrania mwaminifu kutoka kwenye mabaraza mashuhuri ya Sanhedrin, kutoka kwenye sinagogi, kasema, "Sasa, je! chaweza chochote chema kuja kutoka Nazareti?"

139 Unaona jinsi ambavyo Mungu huwanyenyekeza tu watu, huwashusha? Wakati wamejijenga wenyewe kuwa kitu fulani, Mungu huinua maskini kitu fulani ambacho hata hakijui ABC zake, na hudhalilisha tu kitu hicho. Unaona, hivyo ndivyo Mungu afanyavyo. Kwa sababu, Mungu angali ni Mungu, Yeye huchukua kitu duni ili kufanya kitu kutokana nacho. Vipi kama angalikuja kwa Kayafa na makuhani wakuu, na makasisi waliokuwa wamefunzwa kuchukua huduma ya siku hiyo wakati Masihi ajapo? Wangalikuwa na kitu cha kujivunia.

140 Na hebu niliseme, si kuwa fidhuli; ninatumai sieleweki hivyo. Si ingekuwa imetendeka tena? Kwa hiyo kile tunachowazia, "sisi Methodisti tunacho, sisi Baptisti tunacho," na Mungu huenda akainua mtu ambaye hakutoka kwenye shule ya namna yoyote, ama kundi fulani la watu ambao Yeye angeweza kutia upako kwa Roho Wake, ambao hata hawajui ABC zao. Biblia ilisema kwamba "Petro alikuwa ni mtu asiye na elimu wala maarifa." Lakini kile alichokuwa nacho, walikitambua, kwa sababu ilikuwa ni Mungu akiishi kupitia yeye. "Kile nilicho nacho, ninakupa wewe," unaona, kwa yule mtu kiwete.

141 Tunakuta basi katika wakati huu mkuu, kwamba mtu huyu alisema, "Vema, sasa ngoja kidogo, chaweza kitu chochote chema kutoka Nazareti?"

142 Sasa alimpa mtu huyo jibu zuri kwelikweli, alisema, “Njoo, uone.”

143 Usikae nyumbani na kukosoa, njoo ujionee mwenyewe. Usinene au kusema yale mtu mwingine amesema. Njoo, ujionee mwenyewe.

144 Njiani mwake akizunguka mlima, huenda walizungumza kuhusu wakati ambapo—ambapo walikuwa wameenda kununua samaki. Akasema, “Unamkumbuka yule mzee mvuvi ambaye asingeweza kutia sahihi jina lake kwenye risiti, maskini yule mvuvi?”

“Naam, ninamkumbuka. Simoni.”

145 “Vema, alipotembea moja kwa moja kuingia Uweponi mwa—mwa huyu . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . mmiliki wa Uzima wa Milele, mbona, Yeye alimwambia, wakati Yeye akitazama kote pale, ndipo Yeye akasema, ‘Jina lako ni Simoni, na wewe ni mwana wa Yona.’” Unaona? Na yeye akasema, “Unajua kwamba tumefundishwa na kiongozi wetu aliyetuachia neno hili, kwamba katika siku hizi za mwisho, kwetu sisi, ‘atakuja Nabii,’ Bwana atainuka miongoni mwetu.”

“Loo,” akasema, “Ni vigumu kwangu kuamini hilo. Itanibidi niende nione.”

146 Na punde tu alipoingia kwenye kusanyiko; si mkosoaji. Sasa ninatumaini hivyo ndivyo wewe unakuja, asubuhi ya leo; si mkosoaji, kuja tu kuona kama ni sahihi, au la. Akaingia katika kusanyiko, akasimama tu hapo. Na punde tu aliposimama, angalia Chanzo hiki cha Uzima wa Milele, na Chanzo pekee; Yeye aligeuka na kumtazama, ndipo Yeye akasema, “Tazama, yule pale Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.”

147 Akasema, “Rabi,” maneno mengi sana ya hili, “ulinijua lini Wewe? Sijawahi kukuona Wewe, na Wewe hujawahi kuniona. Wewe unajuaje chochote kunihusu mimi?”

148 “Mbona,” Yeye akasema, “kabla Filipo hajakuita, wakati ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Siku moja kabla, na maili kumi na tano kuzunguka milima.

149 Kitu gani? Aliwekeza katika hati ya mkataba moja kwa moja. Alianguka miguuni Pake; mtu huyu mwaminifu, mshiriki wa kanisa. Ni tofauti jinsi gani kati ya huyo na mfanyabiashara kijana tajiri! “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu! Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli!” Upesi alichukua hati ya mkataba.

150 Vipi kuhusu maskini yule mwanamke kisimani? Wao walikuwa ni Wayahudi; hebu twende kwa Wasamaria.

151 Na sasa tuko kwa Mataifa. Wayahudi na Wasamaria walikuwa wakimtazamia Masihi; si Mataifa. Tuliabudu sanamu. Warumi na Wayunani, na chochote tulicho, tuliabudu sanamu. Lakini Wayahudi walikuwa wakimtazamia Masihi, na vivyo hivyo na Wa—Wasamaria, na tunakuta ya kwamba Masihi

hujifunua tu Mwenyewe kwa wale wanaomtazamia. Kama uko hapa asubuhi ya leo, ukimtazamia Yeye, Yeye atajifunua Mwenyewe. Kama humtazamii, Yeye hatajifunua. "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

152 Kwa hiyo Wasamaria walikuwa wakitazamia. Na Yeye alikuwa anaenda Yeriko, bali Yeye alikuwa na haja kupitia Samaria. Na huku ameketi kwenye lango la mji, Sikari, tunakuta kwamba wanafunzi Wake walienda kununua maakuli. Na Yeye aliachwa peke yake.

153 Ndipo ma—maskini mama fulani, maskini mwanamke, na mwanamke mwenye sifa mbaya, hakuwa na fedha zozote. Hakuwa kama yule mtawala kijana tajiri. Kwa hiyo yeye akaja, kitu kimoja pekee tunachojua kuwa alikuwa nacho, alikuwa na maskini chungu cha maji, ndipo akakiweka chini na alikuwa anajiandaa kushusha winchi ndani ya kisima, kuchota maji.

154 Ndipo akaangalia kando yake, katika mandhari ndogo, na hapo aliketi Mwanaume, Myahudi, alionekana, nadhani . . . Biblia ilisema, "Wewe ni Mtu usiyezidi miaka hamsini." Nadhani Yeye alionekana wa miaka hamsini, lakini Yeye alikuwa tu na thelathini na kitu. Na ilikuwa si kawaida kwa Wayahudi na Wasamaria kuwa na ushirika wowote, kwa sababu kulikuwa na ubaguzi.

Kwa hiyo Yeye akasema, "Niletee maji ninywe," kuwasiliana na roho yake.

155 Akasema, "Vema, si kawaida kwenu nyinyi Wayahudi kumwomba mwanamke Msamaria hivyo."

156 "Bali," kasema, "kama ulijua ni Nani unayezungumza naye!" Ndipo basi Yeye akashika roho ya mwanamke huyo, na Yeye akasema, "Nenda kamwite mume wako na mje hapa."

Akasema, "Sina yeyote."

157 Akasema, "Umesema vizuri, kwa kuwa umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa si mume wako."

Hiyo ilimsimamisha. Ilikuwa ni kitu gani? Akasema, "Bwana!"

158 Mnakumbuka Mafarisayo, siku chache kabla ya hapo? Wakimwona Yesu akionyesha hiyo ishara ya Masihi, kwamba Yeye alikuwa ndiye Nabii aliyepaswa kuja, na wao wakasema, "Yeye ni mtu anayewasiliana na mizimu. Yeye ni Beelzebuli, mkuu wa pepo, namna fulani ya mpiga ramli." Iliwabidi kutoa jibu kwa kusanyiko lao, kazi zilikuwa zimefanywa. Iliwabidi kujiondolea aibu mbele ya kusanyiko. Kazi zilikuwa zimefanywa, wasingeweza kukana hilo. Wakasema, "Ni roho mwovu."

159 Yesu alisema, "Ninawasamehe," Mwana-kondoo hakuwa ameuawa. "Lakini ajapo Roho Mtakatifu kufanya jambo lilo

hilo, neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe," unaona, unaona, kwa hiyo hapa tunawakuta katika hali hii.

160 Naye maskini mwanamke huyu hakuwa na chochote. Labda alikuwa amejiepusha na kanisa, alikuwa ameona mengi sana katika hilo. Kwa sababu, chini katika moyo wake kulikuwa na mbegu imelala, Uzima wa Milele; "wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Na punde tu Nuru hiyo ilipoangaza juu yake, yeye hakuita Hiyo ibilisi. Angalia tofauti kati ya mwanamke huyo na makasisi. Alisema, "Bwana, naona kuwa Wewe ni Nabii! Tunajua kwamba Masihi ajapo, hayo ndiyo mambo atakayofanya Yeye. Tunamtazamia Masihi. Hatujakuwa na nabii kwa mamia ya miaka. Lakini kiongozi wetu, Musa, alituambia kwamba kutakuwa na Nabii atakayeinuka katika siku za mwisho, na Yeye atakuwa ni Masihi," ambalo linamaanisha Yule *aliyepakwa mafuta*, mpakwa mafuta.

161 Yeye alikuwa ni Neno. Mungu ndiye Neno, na alikuwa ndani ya Kristo. Nayo Biblia ilisema ya kwamba, "Neno la Mungu, Neno, ni kali, lina nguvu zaidi, na ni kali kuliko upanga ukatao kuwili," Waebrania 4, "lachoma hata kugawanya, mafuta ya mfupa, na Mtambuzi wa mawazo na makusudi yaliyoko moyoni." Hiyo ndiyo sababu Yeye angeweza kuwatazama na kujua kile walichokuwa wakiwazia, kwa sababu Yeye alikuwa ni Neno. Yeye alikuwa ni Uzima. Angali ni Neno, na Yeye angali ni Uzima. Na Yeye alijua! Yeye hufanya jambo lile lile. Sasa tunaona . . .

162 [Dada fulani anatoa himizo, katika kusanyiko—Mh.] Amina. Jina la Bwana libarikiwe, kwa ajili ya ujumbe Wake juu ya hili.

163 Loo, hati hiyo ya mkataba wa Uzima! Uzima! Uzima, kitu kikuu kuliko vyote kilichopo ni Uzima. Na kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, na hiyo ni Mungu.

164 Sasa mwangalie maskini mwanamke huyo, kama unabii ndio kwanza utolewe, kwamba yeye alikuwa na chungu cha maji mkononi mwake. Lakini pia alikuwa na kingine moyoni mwake. Akasema, "Ninaona kuwa Wewe ni Nabii, na sisi tunajua Masihi ajapo, Yeye anaenda ku—kufanya mambo haya. Hayo ndiyo Yeye atakayofanya. Hiyo itakuwa ndiyo ishara Yake iliyothibitishwa. Yeye atakuwa ni Neno, akitambua. Na Wewe umenisomea moyo wangu hasa. U nani Wewe?"

Ndipo Yesu akasema, "Mimi Ndiye."

165 Ndipo chungu *hiki* cha maji kikatulia, bali *hiki* kilijazwa, naye mwanamke huyo akachukua hati ya mkataba wa Uzima wa Milele. Akasema, "Maji ninayotoa ni Uzima wa Milele, yanayobubujika, na kuruka ndani ya moyo."

166 Na ndipo asingeweza kutulia, alitaka wanadamu wenzake pia wawe na hati hii ya mkataba, na chini kupitia kwenye mji alienda. Kusema kweli, yeye hakuwa na haki za kufanya hivyo, alikuwa ni mwanamke mwenye sifa mbaya. Enyi wanaume

na wamishenari hapa mnajua kwamba huko Mashariki hiyo ingali ndiyo... Wasingemsikiza. Bali, wao, watajiepushaje na hilo? Alikuwa amejawa Uzima wa Milele. Iliwabidi kumsikiza. Kama vile nyumba inayoungua moto, kwenye siku kavu yenye upepo, usingeweza kuikomesha. Huyo akaenda! Na si hayo tu, kama hakuwa amejazwa, wanaume wasingalimsikiliza. Lakini alikuwa na kitu halisi alichojua habari zake. Na sisi tunaona, walisema... "Njoni, mwone Mtu ambaye ameniambia mambo niliyofanya. Haimkini huyo kuwa ndiye Masihi?"

167 Ndipo wakamleta ndani ya mji. Hakulifanya hilo tena, bali watu waliamini ushuhuda wa mwanamke huyo. Na wote wakamwamini Bwana Yesu.

168 Upesi sasa, maana ni—ninasikitika kuwaweka namna hii. Lakini kama mtanipatia tu... vumilieni tu dakika zingine chache, nina jambo hapa ninalotaka kusema. Angalia.

169 Nikodemo alikuwa ni mtu mashuhuri, na alikuwa ni mtu wa kidini. Alikuwa mwalimu, mtawala miongoni mwa watu wake, mtu maarufu.

170 Kitu kama Simeoni, kuhani, wakati wa kuzaliwa kwa Bwana Yesu. Aliahidiwa, na Roho Mtakatifu, kutoona mauti mpaka alipoona wokovu wa Bwana; jinsi alivyoongozwa na Roho, kuingia chumbani, kumbariki Mtoto huyo.

171 Jinsi ambavyo Ana, nabii mke, kipofu, huko kwenye kona, hakuondoka, mchana na usiku; lakini wakati uo huo, hakuna mtu aliyewaambia, akiongozwa na Roho Mtakatifu, mwanamke huyo kipofu akipenya kupata njia yake kupitia kwenye watu, na akasimama kando Yake, na kumsifu Mungu kwa ajili Yake. Kama mwanamke aliye kipofu kimwili, alikuwa katika hali mbaya; bali kuna watu New York, asubuhi ya leo, walio vipofu kuliko mwanamke huyo, na wanaweza kuona kwa macho yote mawili. Lakini aliongozwa na Roho, Roho wa Uzima alimwongoza kwenye chemichemi ya Uzima.

172 Kwa sababu unaonea Hiyo kiu, hapana budi kuwepo na Chemichemi mahali fulani. Daudi alisema, "Kilindi, wakati kinapoita Kilindi, lazima kuwe na Kilindi cha kuitikia mwito huo." Kwa maneno mengine, kabla ya kuwa na pezi kwenye mgongo wa samaki, ilibidi kuwe na maji kwanza kwake kuogelea ndani, la sivyo asingalikuwa na hilo pezi. Kabla ya kuweko na mti kumea ardhini, ilibidi kuwe na ardhi kwanza kwake kumea ndani, la sivyo kusingalikuwa na mti. Basi mnaona ninachojaribu kusema, kama inabidi kuwa na... Kwa sababu unaona njaa, asubuhi ya leo, kwa sababu watu wanaona kiu, inaonyesha kuna chemichemi ya Uzima iliyofunguliwa mahali fulani, unaona, kwako kuitikia Hiyo. Lazima kuwe na Kilindi kwanza, kuitikia kilindi kinachoita, unaona, la sivyo mwito huo usingalikuwepo.

173 Hiyo ndiyo sababu watu huenda kujiunga na kanisa na kuweka tu jina lao kwenye kitabu, badala ya kuzaliwa mara ya pili, kuchukua hati ya mkataba wa Uzima. Halafu wanatoka moja kwa moja na kujaribu kunyamazisha miito hiyo mitakatifu, kwa kuvuta sigara, kunywa pombe, na—na kucheza kamari, na kukimbia huko nje, kizinifu. Unaona hapo? Unathubutuje kujaribu kunyamazisha mwito huo mtakatifu wa Mungu, ambao Mungu aliweka humo ndani kumwonea Yeye kiu! Huna haki.

174 Nina kitu kwa ajili yako, asubuhi ya leo, ni Uzima. Huo ndio unaotaka. Ni Uzima.

175 Na huo ni uhai uliopotoshwa. Huo ni mauti. Hapo ndipo mahali Biblia ilisema, "Mwanamke anayeishi katika anasa amekufa angali hai." Unaona? Kwa hiyo huwezi kuishi katika anasa za ulimwengu na kuwa na Uzima wa Milele.

176 Hati ya mkataba ni sahihi, marafiki. Kwa hiyo, Nikodemo, alikuja kuwekeza. Alikuja usiku, bali alikuta benki daima imefunguliwa. Kwa hiyo huenda kumechelewa, lakini ingali imefunguliwa. Imefunguliwa, Yeye, daima, be—benki imefunguliwa kufanya biashara. Na kwa hiyo a—alipata Uzima wa Milele, kwa kumjia Yesu.

177 Hebu tuchunguze tu mtu mwingine, au wawili. Hebu tuchukue Luka 24:49. Wanafunzi walikuwa wamemwamini Bwana Yesu. Na sasa ulikuwa ni wakati wa ahadi, ulikuwa unakaribia. Na kwa hiyo Yesu aliwaambia wanafunzi Wake, wamiliki wa hati ya mkataba, kwamba walikuwa wanaenda kupata mgao wa faida juu ya hii, bali sharti wangoje kwenye mji wa Yerusalemu mpaka Yeye alipoenda kwenye Makao makuu na kutuma Hiyo kurudi kwao, mpaka hundi iliporudi. Alikuwa anaenda juu, Yeye alikuwa ameitia sahihi katika Damu Yake Mwenyewe, na Yeye alikuwa anapaa juu kutuma mgao wao wa faida kurudi, lakini "kungoja" kwa ajili ya mgao wao wa faida.

178 Sasa, hakusema, "Ngojeni dakika tano, na mfishwe moyo." Kama una imani katika Yeye anayezungumza na wewe, Mungu anayezungumza na wewe, Yeye akasema, "Kaeni mpaka," (muda gani? wiki moja, siku kumi, siku tano, chochote kilichokuwa) "mpaka mpokee malipo haya, mpaka mgao wa faida. Kwa kuwa, tazama, nitatuma ahadi ya Baba Yangu juu yenu. Lakini ngojeni katika mji wa Yerusalemu mpaka mpokee Hiyo, mpaka mja—mjazwe na mgao wa faida kutoka Juu, kwa ajili ya hati yenu ya mkataba wa kuniamini Mimi."

179 Loo, enyi Wabaptisti, enyi Wamethodisti, enyi Wapresbiteri! Sitaki nipate msisimko, lakini hili linatosha kumfanya mtu asisimke. Kwa nini msingoje hapo? Wewe ni mmiliki wa hati ya mkataba, bali kuna mgao wa faida katika Hili.

180 Paulo alisema, katika Matendo 19, kwa wale watu wa Baptisti. Mimi ni mbaptisti, mwenyewe, mimi ni mbaptisti mpentekoste. Kwa hiyo wakasema, "Je! mmepokea

Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?" Sasa, tunafundishwa tunampokea Roho Mtakatifu *wakati* tunapoamini, lakini yeye akasema, "Je! mmepokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?"

181 Wakasema, "Hatujui kama kuna Roho Mtakatifu yeyote."

Akasema, "Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani?"

Wakasema, "Tumebatizwa tayari."

182 Akasema, "Huo hautashikilia tena." Basi waliposikia hili . . . "Walikuwa wamwamini Yesu aliyekuwa aje." Basi waliposikia hili, walibatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Paulo aliweka mikono yake juu yao, ndipo Roho Mtakatifu akaja juu yao; nao wakanena kwa lugha na kumtukuza Mungu.

183 Paulo alisema pia, huko katika mlango mwingine, akasema, "Ikiwa—ikiwa Malaika kutoka Mbinguni anahubiri Injili yoyote tofauti na Hii ambayo mmenisikia nikihubiri, na alaaniwe, kama ni askofu, kadinali, chochote kiwezacho kuwa." Naam! "Ikiwa Malaika kutoka Mbinguni," achilia mbali kadinali, au askofu, au mhubiri, "anayehubiri yoyote nyingine mbali na hati hii ya mkataba wa Uzima wa Milele kupitia Yesu Kristo, na alaaniwe."

Ulisema, "Ndugu Branham, unapoteza akili . . . "

184 Ninajua hasa mahali nilipo, unaona. Sijapotea. Ninajua hasa mahali nilipo. Huenda nimesisimkwa, bali kama nilivyosema hapa hivi majuzi usiku . . .

Mtu fulani alisema, "Wewe unashikwa na kichaa."

Nikasema, "Vema, achana tu na mimi, ninajisikia bora hivi kuliko nilivyokuwa vile vingine, kwa hiyo ni—nina Uzima."

185 Kwa sababu, ni Uzima! Ni upumbavu kwa ulimwengu, lakini kwangu ni adhimu. Nimeokoka, ambapo sikuwa nimeokoka. Sasa ninao ufufuo wa Kristo ndani yangu. Na wapo wengine wengi hapa, ndugu, ambao wanajua Kweli hiyo; una Hiyo ndani yako, ufufuo! Naam.

186 Walipanda juu, hawa wamiliki wa hati ya mkataba, kuchukua mgao wa faida. Loo, jamani! Ndugu wahudumu, hebu tufanye hivyo asubuhi ya leo, hebu tuchukue mgao wa faida sasa. "Ahadi," Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, "ahadi ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walioko mbali, Mataifa," sikilizeni kwa makini, ndugu, "hata wale wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu." Na Yeye ana hakika kumwita kila mmoja ambaye majina yao yako kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo. Mgao wa faida, ni kwa ajili ya wote, naam, "Kwa ajili yenu, na watoto wenu, kwa wote walio mbali." Na faida juu ya hati ya mkataba ililipwa, kwenye Siku ya Pentekoste.

187 Sasa, tajiri kijana Paulo alikutana na Yeye yule, kwa kuwa Yeye alibakia yule yule baada ya kifo Chake. Yeye angali yule yule.

188 Sauli wa Tarso, mtu aliyeelimika vizuri, msomi; samahani. Na yeye—yeye alikuwa mtu mzuri. Alikuwa amefunzwa na Gamalieli, mwalimu mashuhuri wa Kiebrania. Wazazi wake walikuwa matajiri. Paulo alikuwa namna ya mtu tajiri. Aliweza kuzungumza lugha nyingi. Alikuwa na elimu. Shauku yake ilikuwa ni kuwa mwa—mwanasheria; mmoja wa wanasheria, au kasisi, au kitu fulani katika...au mwanasheria, hasa, katika kanisa lake. Mwerevu, alijua Neno. Alikuwa tajiri, na yeye alikuwa na shauku zake.

189 Aliposikia kundi hilo la kufanya yasiyofaa, kelele na kupiga mayowe, na kunena kwa lugha, na, mbona, aliwazia, "Hiyo ni ya kuchukiza, kwa jamii ya Yerusalemu. Hiyo inafaa kukomeshwa." Kwa hiyo akapata nyaraka kutoka kwa kuhani mkuu. Yeye—yeye alizunguka akifanya uharibifu mkubwa kwa kanisa. Kwa hiyo akaingia kwa kadinali au askofu, au chochote unachotaka kumwita, kuhani mkuu, na kupata waraka kutoka kwake, akauweka mkononi mwake na kuenda huko chini Dameski.

190 Bali, unaona, kanisa linaonekana kuwa na mamlaka yote, likiwa na funguo za Ufalme, na kila kitu, na wao walikuwa wamemchagua Mathias kuchukua mahali pa Yudasi. Lakini tazama chaguo la kipumbavu awezalo kufanya mwanadamu. Hakuna kitu alichowahi kufanya. Huenda alikuwa ni mtu mwema. Hapana shaka alikuwa ni mtu mwema. Hapana shaka alikuwa ni mtumishi mnyenyekevu wa Kristo. Lakini, unaona, hilo si kila wakati linaonyesha chaguo la Mungu.

191 Mungu alimchagua maskini mpinzani wa kanisa, Myahudi mdogo, mwenye pua iliyopinda, na hasira ya kutosha kupigana na msumeno, na yeye alikuwa...Huyo hapo, njiani mwake akiteremka. Anaenda huko chini na kuwatia mbaroni hao watakatifu wanaojibingirisha. Atawafunga kwa minyororo. Atawafunga. Anayo mamlaka kutoka kwa askofu wake. Anaenda kufanya hivyo.

192 Basi yapata saa tano siku moja, aliangushwa chini, akiwa na karatasi mkononi mwake. Ndipo akaangalia juu, na akaona Nguzo ya Moto. Unajua, i—ilimbidi kutambua Hiyo. Paulo alijua vema kuliko kusujudia sanamu au roho ovu. Lakini akiwa ni Myahudi, alijua kwamba hiyo Nguzo ya Moto ilikuwa ni Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza watu Wake kutoka Misri, na ilikuwa ndiyo Hii hapa.

193 Wakati Yesu alipokuwa duniani, Yeye alisema, "Nalitoka kwa Mungu, ninaenda kwa Mungu." Baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, na kupaa juu; Huyu hapa alikuwa, amerudi kwa Mungu tena, ile Nguzo ya Moto.

194 Ndipo Yeye akasema, "Sauli, Sauli, mbona unanitesa Mimi? Unayo karatasi mkononi mwako. Wewe ni mtu mashuhuri. Umekuja kutoka kwenye shirika fulani, shirika aminifu kuliko yote na—na shirika linaloheshimika nchini. Unayo karatasi

mkononi mwako, lakini unafanya kosa. Mbona unanitesa Mimi?"

195 Mwangalie Myahudi huyu akisema, "Bwana!" Alijua Huyo alikuwa ni Nani. Haya basi, Nguzo ile ile ya Moto iliyomwongoza Musa na kuzungumza! Hakuwa amekuwa na fursa ya kuwahi kumwona Yesu, kwa hiyo akasema, "Bwana, Wewe ni Nani ambaye ninamtesa?"

Ndipo Yeye akasema, "Mimi ni Yesu."

196 Na hapo akiwa amelala chali, unajua, a—alirarua hiyo karatasi, na akasema, "Nifanye nini?"

197 Akasema, "Ninaye nabii hapa chini, na jina lake ni Anania. Sasa wewe nenda chini kwenye mtaa uitwao 'Nyofu,' atakuambia cha kufanya."

198 Kwa hiyo Bwana akanena na Anania. Ndipo akaja, kasema, "Ndugu Sauli, Bwana Yesu aliyekutokea njiani na alikutaka uchukue hati hii ya mkataba, nimekuja kukuletea hiyo, kwa kuweka mikono yangu juu yako." Alikuwa ni mtu aliyebadilika. Angalia tofauti. Kile ninii . . . Unaona?

199 Baada ya Paulo kuona thibitisho dhahiri, kwamba huyu hakuwa ni mtu mwingine ila Mtu yule yule. Mungu na Kristo walikuwa ni Mtu yule yule. Haukuwa ni upumbavu fulani, kwa sababu Yeye aliona kwamba Neno lilikuwa Nguzo ya Moto, lilikuwa limefanyika mwili, kukomboa; na hii hapa ilikuwa imerudi, Nguzo ya Moto tena, kwamba Mungu na Kristo walikuwa ni Mtu yule yule. Na Yeye huyu hapa, na kurudi kama Roho Mtakatifu, sasa anaitwa, kwa sababu Yeye alikuwa amekuwa juu ya mwanadamu. Aliona Hiyo ikitambulishwa wazi, na—na kuthibitishwa. "Bwana, Wewe unataka nifanye nini? Nifanye nini?" Sasa, kumbukeni, huyo alikuwa ni mtu wa kidini, na mfanyabiashara. "Ni nini Wewe ungetaka nifanye?"

200 Ni tofauti jinsi gani iliyokuwepo kati ya mfanyabiashara kijana, tajiri, na jamaa huyu mwingine kijana, Sauli. Moja, gharama ilikuwa kubwa sana.

"Vema," unasema, "Paulo hakuwa na chochote cha kusalimisha."

201 Alikuwa na kanisa lake, ndugu zake. Alikuwa ni mkimbizi kutoka kanisani, baada ya hapo. Ilimbidi kutoroka. Na hatimaye kanisa lake mwenyewe likachukua uhai wake; walimwua. Na sisi tunaona, aliteswa kutoka mji mmoja hadi mwingine, na alipigwa mawe, karibu kufa wakati mmoja, na kadhalika; ndugu zake mwenyewe. Ndipo yeye akasema, "Ningekuwa laana kwa ajili yao." Hakuwadharau. Wakati alipompokea Roho Mtakatifu, anawapenda. Alitaka kuwaokoa. Usijitenge; waendee wa aina hiyo. Paulo angefanyika laana mwenyewe; kwa sababu ilikuwa ni Roho wa Kristo aliyekuwa ndani yake, ambaye alilaaniwa na kutundikwa mtini kwa ajili ya walio Wake Mwenyewe.

202 Na tunaona jinsi ilivyo tofauti kati ya kijana huyu, mtawala tajiri, mfanyabiashara, na Paulo.

203 Ilimbidi Paulo kusalimisha elimu yake, theolojia yake yote ambayo alikuwa amejifunza, kupitia miaka na miaka ya utafiti na mafunzo. Ilimbidi kuisahau yote. Aliwaambia Wakorintho, "Sikuja kwenu na maneno stadi, makuu ya hekima, kwamba imani yenu iwe katika hekima ya mwanadamu. Bali niliwajia kupitia nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu."

204 Hilo ndilo jambo tunalohitaji leo hii, enyi marafiki. Hiyo ndiyo hati ya mkataba ninayozungumzia. Si kujiunga na kanisa, au kutia mkono wako kwenye kile; sina chochote dhidi yake, hiyo ni sawa. Lakini hii ni saa nyingine, hayo ndiyo yote ninayojaribu kuwauzieni. Kujiunga na kanisa fulani . . . Ninajaribu kuwaambia kwamba kuna hati ya mkataba na chemichemi iliyofunguliwa kwa ajili ya dhambi na uchafu. Dhambi ni nini? Kutokuamini! Kutokuamini kitu gani? Neno! "Yeye asiyeamini amehukumiwa tayari." Kweli.

205 Tazama ni uamuzi wa kijinga jinsi gani. Yeye ni kama watu wengi wa leo hii, wa mawazo yanayopendwa na watu, huyu kijana alikuwa. Aliondoka. Badala ya kulitilia maanani, alipoteza hati yake ya mkataba. Sasa tunafunga.

206 Je, yeye, hivi bahati mbaya ilimwangukia? La. Bahati nzuri ilimwangukia. Tunamwona, mahali pengine, alikuwa na fedha nyingi sana mpaka ilimbidi kujenga upya maghala yake. Na hata alisema, "Nafsi, pumzika."

207 Sasa tunaona, hapo ndani, hakuwa jamaa mbaya. Walipokuwa na mnada au karamu ya kanisa, au kitu fulani, walio maskini katika roho walikaa langoni, huyo alikuwa ni mmiliki wa hati ya mkataba ambao alikuwa ameukataa; aliyafagia makombo machache, na kumpa sadaka fulani ya umishenari, au kitu fulani. Hakuwa jamaa mbaya. Unaona, aliyafagia makombo kuwapa wale walioteswa. Akasema, "Loo, nilihudhuria mmoja wa mikutano yao, nadhani ni sawa. Hakuna chochote hasa ninachoweza kusema dhidi ya watu hao." Kufagia makombo machache, bali hilo halikufanya kazi. Hatimaye, malipo yake yalifika.

208 Basi kumbuka, rafiki, malipo yanakuja kwangu na kwako. Yanakuja kwetu sote. Ninataka mwazie kwa makini sana sasa, katika kufunga.

209 Malipo yake yalikuja, hakika. Alikuwa na ibada kubwa ya mazishi, hapana shaka makasisi fulani waliofunzwa vizuri walikuja na kuzungumza. Haijalishi, nadhani, alikuwa na Wafanyabiashara Wakristo kama wabeba jeneza. Na yeye alikuwa na watu maarufu wa nchini huko nje, na labda afisa wa serikali hata wakampandishia bendera nusu mlingoti. Wakubwa wote walikuwa pale. Naye mchungaji, hapana shaka, ama mtu huyo, kasisi, yeyote yule aliyehubiri mazishi yake, alihubiri

ma—mahubiri ambayo yangewagusa watu kwa jinsi mtu huyu alivyokuwa mashuhuri, "Hata kwa maskini mtaani, alitoa. Loo, ndugu yetu yuko Mbinguni, leo hii."

210 Lakini Yesu alisema, "Aliinua macho yake kuzimuni, na kumwona mmiliki wa hati ya mkataba wa Uzima wa Milele, huko mbali kifuani mwa Ibrahimu, ambaye alikuwa ameandamana na wachache wa Bwana waliodharauliwa."

211 Kama Yesu alivyosema, "Heri ni nyinyi watu wakatapowaudhi," katika mlango wa 5 wa Mathayo, "kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili ya Jina Langu. Heri walio maskini katika Roho, maana Ufalme ni wao. Heri wapole, watamiliki nchi. Na wewe ndiwe mmiliki wa hati ya mkataba wa Uzima wa Milele."

212 Hata hivyo alibaki kuwa mshiriki wa kanisa, unaona. Sasa tazama. Unasema, "Je, alifanya hivyo?" Naam. "Unawezaje kuthibitisha hilo, mhubiri?"

213 Hili hapa. Akasema, "Baba Ibrahimu! Baba Ibrahimu, ninakuomba wewe umtume huyo mmiliki wa hati ya mkataba hapa chini, na maji kidogo tu. Miale hii inatesa."

214 Mwangalie Ibrahimu. "Mwanangu," aliyekiri kuwa Mkristo, aliyekiri kuwa mwaminio, kama ambavyo tungeliita, unaona, "ulikuwa na nafasi yako. Ulipewa nafasi ya hati ya mkataba wa Uzima wa Milele, ambayo ingekupatia hakikisho la kuja hapa, lakini u—ulikatalia mbali Hiyo. Usingeichukua Hiyo. Na sasa mtu huyu, maskini, hata hivyo alikubali Hiyo. Sasa yeye amefarijika, na sasa wewe ndiwe ombaomba."

215 Loo, msiache hili liwatokee, enyi rafiki. Usifanye, usifanye. Usifanye lilo hilo kos-. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . njia hakikisho liwezayo kuja ni kupitia Kristo. Hakikisho kwamba umeokoka, kwamba wewe ni mmiliki wa hati ya mkataba. Sasa, kama huna hiyo, kwa nini usiichukue?

216 Huenda ukawazia, vema, kama vile kijana huyu alivyosema asubuhi ya leo, "Ni—niliingia katika sehemu hizo na wote. . . Nilikuwa mfanyabiashara mashuhuri, na kuinama, na mambo kama hayo." Usiangalie hiyo.

217 Mchezaji kijana hivi majuzi tu alichukua ziara kwenda Urusi. Alikuwa mwimbaji. Na hakika ali—aliwapendeza sana Warusi. Na kwa hiyo watu wote walikuwa wakipiga makofi na kuendelea namna hiyo, wakati kijana huyo alipokuwa amepiga muziki wake. Na walifurahishwa mno, wakakanyaga kwa kishindo kwa miguu yao na kupiga makofi, lakini kijana huyo kamwe hakuvutiwa na kushangilia huko kote. Na kwa hiyo walishangaa ni kwa nini. Kwa hiyo tena wakawazia, "Labda haelewi," kwa hiyo wote walipiga makofi yao tena kwa sauti kubwa mno, na kumshangilia. Wao. . . Alikuwa amefanya kazi nzuri sana. Lakini waliona, yeye—yeye tena, hakutambua kushangilia kwao. Na wao waliona alikaza macho yake juu

kwenye roshani kila wakati; wakaja kugundua, mwalimu aliyekuwa amemfunza. Hakuwa anajali yale watu waliyosema; alikuwa anaangalia kile mwalimu alikuwa aseme juu yake.

218 Na mimi nafikiri, leo hii, rafiki, badala ya kutokeza kifua chetu mbele na kusema, “Sisi ni wafuasi wa kanisa.” Hebu tuangalie juu na kuona kile Mwalimu anachosema kukihusu. Unaona?

219 Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu. [Ndugu mmoja ananena kwa lugha nyingine. Dada fulani anatoa tafsiri—Mh.]

220 Huku tumeinamisha vichwa vyetu sasa, mioyo yetu imeinamishwa, toa tu nafasi, dakika moja ama mbili. Sijui, asubuhi ya leo, kwa uaminifu wote sasa, bila usumbufu wowote, wazia tu kwa dakika moja. Je! umepata Baraka hii kuu? Je! unamiliki hati hii ya mkataba wa Uzima, ushuhuda wa Roho Mtakatifu kwamba maisha yako yamemgeukia Kristo, na Kristo yuko ndani yako?

221 Kama nilivyosema katika Ujumbe; kama Beethoven alikuwa ndani yako, ungefanya kazi za Beethoven, ungeishi maisha ya Beethoven. Usingefanya chochote kingine. Usingefanya chochote kingine ila kutunga nyimbo. Na wewe ungekuwa mtunzi mashuhuri, Beethoven, maana yeye yuko ndani yako. Huyo ndiye ambaye ungekuwa. Ungekuwa Beethoven aliyechukua mwili mwingine.

222 Na ikiwa Kristo yuko ndani yako, utakuwa Uhai wa Kristo, mpenzi wa Neno. Hakuna kitu kinachoweza kusimama na kuchukua mahali pa Neno, maana Yeye ni Neno. Yeye hawezi kulikana Neno Lake Mwenyewe na abaki Mungu.

223 Na wewe hujampokea Kristo moyoni mwako. Umekuwa mshiriki wa kanisa. Sasa, kwa hakika, sina chochote dhidi ya kanisa, na dhidi ya taasisi kubwa kubwa na madhehebu, na mifumo, bali ninajaribu kusema hilo si jawabu. Imethibitishwa hilo silo jawabu. Kristo ndiye jawabu, Utu wa Kristo. Na ikiwa hujampokea Yeye ndani ya maisha yako, asubuhi ya leo, na ungependa tukukumbuke katika maombi, sijui kama utafanya tu hivyo kwa unyenyekevu. Hatuna nafasi kwa ajili ya mwito wa madhabahuni. Bali, unajua, ikiwa wewe . . . Ninaamini kama ungeweza tu kusimama, unajua, na kusema, “Niombee,” wakati unaposimama, nami nitaomba. Kama unaamini kwamba Mungu atasikia maombi yangu, ni—ni . . . na wewe ni mwaminifu katika hilo, ninaamini kwamba Yeye atayasikia.

224 Na nyinyi katika kumbi, na mliosongamana karibu na milango, na kadhalika, haijalishi mahali ulipo, kwenye roshani, kwenye vipandio, ikiwa tu utasema, “Ninamtaka Kristo anikumbuke sasa, kwamba ninataka Uhai Wake ndani ya wangu. Nina hakika kwa matendo yangu, ni—nina hakika kwa namna ninavyofikiria na mambo ninayotenda, kwamba ninataka kuwa

hivyo, ila sijafikia hapo bado. Kwa—kwa kweli ninataka hati hii ya mkataba, Ndugu Branham. Kweli, ninataka Hiyo. Basi wewe—wewe mwombe Yeye kama ninaweza kupata Hiyo. Niko tayari kupokea Hiyo."

225 Je! unaweza tu kusimama kwa miguu yako, na kwa hiyo niweze kuomba pamoja na wewe? Ninii tu. . . Na Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, endeleeni tu kusimama kwa muda mfupi. Endeleeni tu, simameni. Unasema, "Ni—nina haja, Ndugu Branham. Ni—nina nafsi, na i—inanibidi kuondoka. Huenda nikaondoka hata leo, na inaenda kunifaidi nini kama sijajazwa na Uzima huo?" Kwa sababu, kumbuka, uhai wowote mwingine hauna budi kuangamia; ulikuwa na mwanzo.

226 Unasema, "Vema, nimekuwa mshiriki wa kanisa fulani, kwa miaka." Hilo ni jema sana. Ninathamini hilo. Bali hilo silo ambalo ninazungumzia sasa hivi.

227 Je! wewe ni mmiliki wa Uzima wa Milele? Hivi unaweza tu kusimama, juu kwenye roshani, kote hapa mbele, na kulia na kushoto? Mungu akubariki. Simama.

228 Nyinyi ambao mmesimama tayari kwenye kumbi, kama mnaweza tu kuinua mikono yenu; kusudi utambulisho fulani, kitu ambacho unaweza kufanya, kujiingiza katika mwendo, "Nimekubali Huo, mimi mwenyewe, asubuhi ile." Mungu akubariki. Vema.

229 Na kote kwenye vipandio na popote ulipo, inua tu mkono wako na useme, "Nikumbuke, Ndugu Branham. Mimi—mimi ni. . . Kwa kweli ninataka Uzima wa Milele."

230 Sasa wazieni kwa makini sana. Huu, huu huenda ikawa ndio wakati ambapo hilo litatatuliwa. Nita—nitakuwa mwaminifu, rafiki, huu ni Uzima kwangu. Na ni—ni—ninajua kwamba ni kweli. Ni kweli.

231 Je! huenda kuna wengine zaidi? Inaonekana tu kama kulikuwa na wengi zaidi ya hao walioinua mikono yao muda mfupi uliopita. Sasa kama huna hakika, naomba ufanye tu kiasi hicho, simama tu kwa miguu yako, na useme, "Nikumbuke katika maombi yako, Ndugu Branham, unapoomba." Vema. Ni wangapi zaidi? Simama moja kwa moja kwa miguu yako, haijalishi wewe ni nani, simama tu na useme, "Niombee, ndugu." Mungu akubariki. Ninawaona, kupitia kwenye roshani na kote. Sasa mna hakika hao ndio wote? Mungu awabariki. Kundi jingine lilisimama. Je! huenda kuna wengine zaidi sasa? Simama tu kwa miguu yako. Sema . . .

232 Sasa ninajua tumechelewa, naye Roho Mtakatifu ametukatiza mara kadhaa. Vema, hilo ni la ajabu, tunapenda Roho Mtakatifu afanye hivyo, unaona, mradi tu Yeye analeta Neno Lake. Hiyo inaonyesha si tu neno langu, bali Hilo ni Lake, pia. Vema.

233 Sasa hebu tusimame, unaona, kila mtu ambaye hajajazwa na Roho Mtakatifu, ambaye unajua hakuna thibitisho maishani mwako kwamba umejazwa na Roho Mtakatifu, na wewe unataka Huyu.

234 Sasa huenda ikawa wewe ni mshiriki mwema, mwaminifu wa kanisa. Na hilo, loo, jinsi ninavyothamini hilo, hakika. Wewe endelea tu moja kwa moja kanisani mwako. Hilo ni sawa. Kwa sababu, wanawali wanaolala wanaamka sasa, mnaona hilo. Pia kumbukeni, Yesu alisema, wakati mwanamwali aliyelala . . . yule ambaye alijaribu kuishi maisha mazuri kwa nafsi zao, walikuwa ni wanawali, bali hawakuwa na Mafuta yoyote. Mafuta huwakilisha Roho. Hiyo ndiyo sababu tunapaka kwa mafuta, unaona. Mafuta ni mfano wa Roho. Walikuwa ni watu wema, watu wazuri, washiriki wa Methodisti nzuri, Baptisti, Lutheri, namna zote za makanisa, bali hawakuwa na Mafuta.

235 Na wao walikuja katika zamu ya mwisho, Wakati wa Saba wa Kanisa, kununua Mafuta. Na walipokuwa katika harakati za kununua Mafuta, kulifanyika nini? Bwana-arusi akaja. Sasa, hilo lilisomwa tu katika Maandiko, muda mfupi uliopita, na mhudumu huyu mashuhuri hapa. Na hivi hamwoni, je! kuliwahi kuwa na wakati kote kupitia wakati, enyi Wapentekoste? Kote kupitia wakati, hakujawahi kuwa wakati ambapo Methodisti, Baptisti, na Presbiteri wamewahi kulia kwa ajili ya Roho Mtakatifu kama wanavyofanya sasa hivi. Unaona? Na wanapofanya hivyo, hicho ni kitu gani? Alikuja moja kwa moja wakati huo! Hiyo ilikuwa ndiyo saa ya Kuja Kwake. Na moja kwa moja wakati wao, hawa ndugu wote na makanisa yanapoona njaa, inabidi . . . Mwanamwali huyu anainuka, mnajua, katika Siku ya mwisho, kwenye Hukumu, Kiti Cheupe cha enzi; bali si Bibi-arusi.

236 Sasa ikiwa huna Mafuta katika taa yako, wakati milango ya rehema, natumai, ingali wazi, hivi hutasimama, na useme, "Nikumbuke, Ndugu Branham." Katika kufanya hivyo, itamwonyesha Mungu, "Nita . . . Mafuta yangu ha—hayako kwenye taa yangu, Ndugu Branham, ni—ninamwamini Kristo. Hakika, ninamwamini. Nimekuwa mshiriki kwa muda mrefu. Lakini kwa kweli kusema maisha yangu yamejazwa na huyo Roho Mtakatifu mpendwa, na kila kitu ni tofauti, na mimi ni kiumbe kipya, siko hivyo, Ndugu Branham. Niombee." Mungu awabariki sasa. Wapo wengi, wengi ambao wamesimama, kwenye roshani na kila mahali.

237 Sasa ninawatakeni enyi ndugu wahudumu hapa, ndu—ndugu zangu wa thamani, kuomba pamoja nami sasa tunapoomba, kila mmoja wenu.

238 Ulisimamaje wakati ulisimama? Unaona, wewe ni uhai. Kitu fulani kiko ndani yako. Kama hakukuwa na uhai, usingaliweza kusimama. Na kulingana na sayansi, unaona, nguvu za uvutano

zingekushikilia chini. Lakini ro—roho fulani ndani yako alifanya uamuzi, kwa ushahidi wa Roho mwingine, Uhai unaosema, “unanihitaji Mimi,” ndipo ukasimama. Ulikiuka kanuni za maumbile, kwa kusimama, kama shahidi. Yesu alisema, “Yeye atakayenishuhudia Mimi, kwa maneno mengine, mbele za watu, huyo nitamshuhudia mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu.” Sasa mnahitaji Roho Mtakatifu.

239 Sasa kama baadhi yenu enyi watu mnaosimama karibu na watu hao ambao wamesimama, ambao mna ubatizo wa Roho Mtakatifu, hivi mnaweza . . . Siwezi kuwafikia wote, hatuna wakati. Kwenye roshani, ndani kila mahali, naomba msimame tu na kuweka mikono yenu juu yao, unaona, katika ukumbusho.

240 Unajua, wao, wakati Filipo alipoteremka huko chini kuwahubiria Wasamaria, walikuwa hawajapokea Roho Mtakatifu bado, unaona. Ila tu, Filipo alikuwa amewabatiza katika Jina la Yesu Kristo, lakini Roho Mtakatifu hakuwa amekuja juu yao. Ndipo Petro na Filipo wakaenda huko chini, ama . . . Petro na Yohana wakaenda huko chini na kuhubiri, na kuweka mikono juu yao, na Roho Mtakatifu akaja juu yao.

241 Sasa nyinyi waaminio ambao mmepokea Roho Mtakatifu, angalia ni nani aliyesimama, kote karibu nanyi, halafu mweke mikono yenu juu yao kama kumbukumbu kwamba wewe ni mwaminio, gusa mikono yao au kitu fulani wakati tunapoomba. Msitie shaka. Aminini sasa. Si mhemuko, ni utamu wa Roho Mtakatifu ambao unashuka na kujaza kila maisha. Sasa wako mikononi mwenu. Mmefanya uhusiano na wao. Kama tu vile wakati mnapoweka mikono yenu . . .

242 Myahudi aliweka mkono wake juu ya sadaka, kujiunganisha mwenyewe na sadaka hiyo. Siku moja uliweka mikono yako juu ya Yesu na kujiunganisha mwenyewe na Sadaka. Uhai wa Sadaka umerudi juu yako. Ambao, huenda nikazungumza usiku wa leo kanisani, “ile Ishara,” na Hiyo iko juu yako sasa.

243 Na wewe umejiunganisha mwenyewe na mwanamume huyu au mwanamke ambaye anataka kuamini. Simameni tu moja kwa moja sasa na mweke mikono yenu juu ya wale wanaotaka kupokea Hiyo. Hiyo ni kweli. Mungu awabariki. Ni wakati mzuri jinsi gani! Sasa usitie shaka. Usiwe na pupa. Kumbuka tu, mwombee mtu huyu.

244 Na wewe omba, pia, useme, “Bwana Yesu, maskini moyo wangu una njaa. Ninakutaka Wewe moyoni mwangu. Ninakutaka Wewe maishani mwangu. Nijaze, Bwana. Nipo hapa, tayari.”

245 Baba yetu wa Mbinguni, wote waliosimama kwa miguu yao, wanaonyesha kwa hili kwamba wanataka Uzima. Na Uzima huja tu kwa kumtii Kristo. Yeye ni Uzima. Anayo masharti ambayo hatuna budi kutimiza. Na kwa kutimiza masharti haya . . . Tunapowazia kuhusu Ibrahimu, alimwamini Mungu, na

ilihesabiwa kwake kuwa ni haki. Na baada ya kuhesabiwa kwake kuwa haki, Mungu alimpa muhuri wa tohara, kama thibitisho kwamba Yeye alikuwa amepokea imani yake. Wengi wa watu hawa wanakiri kuwa na imani, lakini hawajatiwa muhuri bado na Roho Mtakatifu. Na sasa wamesimama, Bwana, kama kumbukumbu ya kwamba wanaamini. Sasa watie muhuri, Bwana, kwa Roho Mtakatifu. Jalia Huyo ashuke juu yao na kutia muhuri kila moyo hapa sasa hivi. Jalia Roho Mtakatifu ashuke katika bwalo hili la dansi, kwenye wakati huu tu.

Na, Shetani, wewe toka katika maisha yao, waachilie.

246 Pia jalia nguvu za Yesu Kristo aliyefufuka zije juu ya watu hawa sasa hivi, na ninaomba wajazwe na nguvu na ufufuo wa Yesu Kristo. Amina.

*Uwekezaji* SWA63-1116B
(Investments)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi asubuhi, tarehe 16 Novemba, 1963 kwa ajili ya kiamshakinywa cha Ushirika wa Kimataifa wa Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Hoteli ya Statler huko New York, New York, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org